Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Tatu – Tarehe 12 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE)**

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2007 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2008/2009.

Taarifa ya Sera za Fedha kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2008/2009.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA 38

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo kwa Mujibu wa Kanuni ya 38 kwa kuwa ni Alhamisi na Bunge linakaa ilikuwa inabidi tuwe na Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nadhani kutokana na hali halisi ya siku ya Bajeti na vikao ambavyo Waheshimiwa Mawaziri wanakuwa navyo kuhitimisha suala la Bajeti itakuwa vigumu sana kuwa na Maswali kwa Waziri Mkuu siku ya Bajeti inapoangukia kuwa ni siku ya Alhamisi.

Kwa hiyo, jana Mheshimiwa Naibu Spika, aliwatangazia na leo itabidi niwahoji rasmi kwa sababu ni matakwa ya Kanuni ya 38 ili tuweze kumruhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu akaendelee na vikao au ajiandae kwa vikao vinavyohusiana na Bajeti leo saa 10.00 jioni. Kwa hiyo, hoja naiweka mbele yetu hapa ni kutengua Kanuni ya 38 ili kipindi cha maswali kiwe na maswali ya kawaida yaliyopangwa, na baada ya hapo tutaona namna ya kuiweka hii Kanuni ili siku ya kusoma bajeti inapoangukia siku ya Alhamisi basi tuweze kuwa na utaratibu tofauti. Kwa hiyo, sasa nitawahoji kwa hoja hiyo. Wanaoafiki waseme ndiyo, ndiyo, wasioafiki waseme siyo. Walioafiki

wameshinda. Kwa hiyo, hatutakuwa na kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu. Ahsanteni sana.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki Hoja ya Kutengua Kanuni ya 38)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 21

### Magari ya Kuzolea Taka

**MHE. MWAKA ABRAHAM RAMADHAN** aliuliza:-

Kwa kuwa utunzaji wa mazingira ni muhimu; na kwa kuwa, magari yanayozoa takataka Mijini huchafua mazingira na kusababisha usumbufu kwa wananchi kwa kutoa hewa chafu wakati wa mchana:-

(a) Je, kwa nini takataka zisizolewe usiku?

(b) Je, kwa nini yasitafutwe magari maalum ya kuzolea takataka tofauti na hayo ya kawaida yanayotumika kwa kazi hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhan, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mazingira ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu na ustawi na maendeleo ya jamii. Ni kweli kabisa kuwa baadhi ya magari ambayo yanatumika katika kuzoa taka husababisha uchafuzi wa mazingira kwa kuwa hutoa hewa chafu na hudondosha taka ovyo. Hoja ya Mheshimiwa Mbunge ya kuzoa taka usiku ni hoja ya msingi, kwani Majiji na Miji mingi katika nchi zilizoendelea hutumia utaratibu huo. Kwa hapa kwetu kuna baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam ambayo kazi ya uzoaji taka hufanyika wakati wa usiku.

Hii ni kutokana na mazingira ya maeneo hayo na huduma nyingine ambazo huwezesha kazi hii kufanyika kwa ufanisi zaidi wakati wa usiku. Hata hivyo, kwa kuzingatia hali ya usalama wa watumishi, ukosefu wa taa barabarani na hali ya vitendea kazi ilivyo hivi sasa, itakuwa vigumu kwa Halmashauri zote za Miji, Manispaa na Majiji ambazo ndizo zenye majukumu ya kuhakikisha kuwa taka zinazolewa, kuzoa taka wakati wa usiku.

Hivyo basi tunashauri kuwa mbinu mbalimbali ziendelee kutumika kuboresha hali ya sasa kama vile kuzoa taka mapema kabla hazijaoza, kutenganisha taka mahali zinapozalishwa na kufunika taka kwa nyavu wakati wa kuzisafirisha. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa Mkakati wa Usimamizi wa Taka unaolenga kuimarisha usimamizi wa taka na kupanua ushiriki wa wadau katika suala zima la huduma za taka. Mkakati huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2008/2009.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba maeneo mengi ya Miji hutumia magari ya kawaida tofauti na magari maalum ya kuzolea taka, hii hutokana na ukweli kwamba magari maalum ya kuzolea taka ni ghali mno kiasi cha kuhitaji fedha nyingi kwa ajili ya ununuzi wa magari haya huwa hazipo katika baadhi ya Halmashauri zetu. Hata hivyo baadhi ya vifaa na magari yanayotumika hivi sasa katika Manispaa na Majiji vinakubalika kitaalamu katika Miji mingine duniani. Ili kuhifadhi mazingira na kulinda afya ya jamii, Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji kwa kushirikiana na Serikali Kuu zitaendelea kuboresha upatikanaji wa vifaa mbalimbali na magari maalum ya kuzolea taka na kuhakikisha kuwa kiwango cha uzoaji taka kinaboreshwa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ninalo swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mbali na usumbufu na uharibifu wa mazingira unaopatikana wakati wa kuzoa taka, lakini hata katika madampo yenyewe ya kuwekea taka nako vilevile kuna matatizo. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuzitumia taka hizo kuzalisha umeme kama teknolojia ambazo zinafanyika katika sehemu nyingine za duniani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba taka hizo ambazo huwa zinatumika hasa taka ngumu uweza kutumika kwa ajili ya uzalishaji wa gesi. Tunao tayari mradi mmoja ambao ni mradi wa bia kati ya Manispaa yetu ya Ilala pamoja na Kampuni kutoka Italy ambayo ina lengo la kuzalisha umeme wa megawati 2.5 kwa ajili ya kuuingiza katika grid ya Taifa. Lakini mbali na pale wataweza kuuza *Carbon Trade* katika soko la Kimataifa. Tunaendelea kuzishawishi Halmashauri na Majiji kuweza kutumia fursa hii ya rasilimali ya taka ngumu kwa ajili ya kuweza kutengeneza nishati na vile vile kuweza kushiriki katika soko la *Carbon Trade.*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa uchafuzi wa mazingira haupo kwenye Miji yetu tu, hata kwenye barabara kuu pale magari yanapopata *breakdown* yanakata matawi makubwa na kuyaweka barabarani kama ishara ya kutokugongwa na kuweka mawe makubwa, lakini pale wanapomaliza matengenezo huondoka na kuacha uchafu pale pale. Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kumekuwa na uchafuzi mkubwa hasa katika maeneo ya barabara kwa ajili ya wale wanaotengeneza barabara, kukata miti ovyo na kuweka matawi barabarani, lakini pia kwa wasafiri wanapotupa chupa nje pamoja na maganda ya ndizi na taka zingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa ya Bunge hili Tukufu kutoa tamko katika Bunge hili kwamba kuanzia sasa tumezidi kutoa elimu. Lakini kuanzia sasa napenda wananchi wafahamu kwamba Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inatoa kifungo kwa ajili ya wale watu wanaotupa taka ovyo cha kuanzia miezi 6 mpaka 12. Lakini unaweza ukatoa faini ya mpaka shilingi milioni 1,000,000 kwa ajili tu ya utupaji taka.

Kwa hiyo, tunaomba wananchi wajue kwamba sheria ni ngumu, tutakapopata tu *Environmental Inspectors* ambao tayari tupo katika hatua ya kuwapata, basi watu watashikwa huko na wataweza kufikisha Mahakamani. *(Makofi*)

Na. 22

**Malipo ya Mishahara kwa Walimu wapya**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilitoa kibali cha kuajiriwa kwa Mkataba wa miaka miwili walimu 75 kupitia barua namba CB/207/237/107 ya tarehe 7/6/2007; na kwa kuwa, walimu hao walipangwa kwenye shule mbalimbali za Halmashauri ya Moshi Vijijini:-

(a) Je, ni lini walimu hao watalipwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, ni dhuluma kuwatumikisha walimu hao bila kuwalipa?

(c) Je, Serikali iko tayari kuwalipa mishahara yao pamoja na riba kwa viwango vya benki?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu ilipata kibali cha kuajiri kwa Mkataba walimu wastaafu 250, ikiwa ni mojawapo ya hatua za kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu katika shule za sekondari. Walimu hao waliajiriwa mwezi Januari, 2007 na kupangwa kufundisha katika shule za sekondari zilizo karibu na wanakoishi katika Mikoa yote. Walimu wote walioripoti walikwishaingizwa kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali (*Payroll*).

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya walimu katika shule za sekondari za Kata, Halmashauri ziliomba kuajiri walimu wastaafu zaidi kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kupewa kibali cha kuajiri. Mawasiliano yamefanyika kati ya Wizara na *TSD* ili walimu wa Halmashauri ya Moshi (V) na Halmashauri nyingine zenye walimu kama hao waingizwe kwenye *Payroll* katika mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, siyo nia ya Serikali kuwatumikisha walimu bila malipo. Hivyo utaratubu wa kuwaingiza kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali *(payroll*) utakapokamilika walimu hao watalipwa malimbikizo ya mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kuwalipa walimu hao kwa kuzingatia taratibu na kanuni za malipo ya fedha kwa watumishi wa umma.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba ni kweli walimu hao wameajiriwa na wanafanya kazi. Serikali haioni kwamba ni makosa kumtumikisha mtumishi kwa miaka zaidi ya mmoja bila kuwalipa. Je, mtumishi huyo akifanya makosa ya udokozi kwa kukosa fedha za kumwezesha kuishi, Serikali haioni kwamba ndiyo inayosababisha matatizo hayo kwa watumishi ambao wanafanya kazi bila kuwalipa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kosa la jinai kufanya udokozi kwa mtu yeyote yule na siyo walimu tu.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba walimu wake wa Jimbo la Vunjo pamoja na walimu wengine tuliowaajiri kwa Mpango wa *TSD* watalipwa kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa malipo ya walimu kutolipwa kwa muda imekuwa kero sana kwa walimu na kwa jamii nzima; na kwa kuwa malipo yao ya gharama za matibabu, nyongeza kwenye mishahara na fedha za likizo hazilipwi mpaka pale walimu wanapotishia kugoma, na hata mwaka huu walitaka kugoma.

Ningependa kuelezwa je, Wizara sasa imejiandaa namna gani kuhakikisha kwamba matatizo kama hayo hayatokei tena?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, alichosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, lakini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kweli inajitahidi sasa hivi kuwalipa walimu, na walimu ni wengi katika nchi hii, na siyo kuwalipa walimu wote kwa wakati kwa sababu wana matatizo wao wenyewe wanapowasilisha yale madai. Tangu tuwambie walete vielelezo vya madai yao wengine mpaka sasa bado havitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi walimu wetu wanalipwa na tuna uchungu nao kwa kazi wanayoifanya, na tutaendelea kuwalipa kadri tunavyopata vielelezo halisi vinavyohusu madai yao.

Na. 23

**Huduma za EMS**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa siku za hivi karibuni huduma ya *EMS* kwenye Shirika la Posta zimezorota kiasi cha kuchukua zaidi ya siku tatu kabla ya mteja aliyepelekewa fedha kwa njia hiyo ya *EMS* kupata fedha hizo; na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha usumbufu kwa wateja kufuatilia fedha hizo kwa kwenda mara kwa mara ofisi ya Posta na kuwasiliana kwa simu na mtu aliyetumia fedha hivyo kuingia gharama nyingine za nauli na simu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, Shirika la Posta linafanya makosa makubwa kwa kutoweza kutekeleza huduma hiyo kwa kasi inayotarajiwa na bila usumbufu kwa wateja wake?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuliwezesha Shirika hilo kutoa huduma hiyo kwa kasi na kiwango kinacholingana na gharama na matarajio makubwa kuhusu huduma hiyo?

(c) Je, Serikali haioni kuwa, ni vema kuibinafsisha huduma hiyo na kuleta ushindani utakaoleta huduma bora kwa wananchi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge hili baada ya uteuzi uliofanyika katikati ya mwezi Mei, 2008. Napenda uniruhusu nichukue dakika moja nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Aidha, napenda kumshukuru sana kwa imani aliyokuwa nayo kwangu ikiwa pamoja na ile ya Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa kuniamini kwamba nitatekeleza majukumu ya Wizara hii mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe, kuwashukuru Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambao mmenipa nikiwa katika Wizara mbalimbali na mategemeo yangu ni kwamba tutaendelea kushirikiana vilevile katika Wizara hii mpya.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vilevile kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Uchaguzi wa Kilolo Mkoani Iringa kwa imani ambao wameendelea kuwa nao kwangu, na vilevile kwa ushirikiano ambao wananipa, kwani bila kunifikisha hapa wao nisingeweza kuonekana mbele ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mwisho, na siyo kwa mpango napenda sana kumshukuru mke wangu Violet pamoja na Ndugu zangu ambao kila wakati wamekuwa pamoja nami katika kunipa moyo ili nitekeleze wajibu wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache. Sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania hutoa huduma ya *"EMS Money Fax"* kupitia mtandao wake na hivi sasa huduma hii, hupatikana katika vituo 124 vilivyoko sehemu mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na malalamiko ya ucheleweshaji wa malipo katika baadhi ya vituo na hivyo kuleta kero kwa wananchi. Hali hii imesababishwa na mtaji mdogo ndani ya ya Shirika la Posta jambo ambalo linafanya Shirika la Posta lisiweze kuwa na fedha za kutosha katika kila kituo kinachotoa huduma hii.

Hali hii inapojitokeza inabidi fedha zihamishwe kutoka kituo kimoja hadi kingine na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa malipo kwa wateja.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza mchakato wa kuliwezesha Shirika la Posta Tanzania ili liweze kujiendesha kibiashara zaidi na tayari Baraza la Mawaziri limefanya maamuzi ya kufuta na kuchukua baadhi ya madeni makubwa yanayolikabili Shirika hilo pamoja na kuchukua jukumu la kulipa pensheni za wastaafu kwa wafanyakazi ambao ajira zao zilianza lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, maamuzi haya yakitekelezwa kikamilifu Shirika la Posta Tanzania litakuwa na uwezo zaidi wa kuendesha shughuli zake kwa ufanisi. Aidha, Serikali ikikamilisha mchakato wa kufuta na kuchukua madeni na pensheni, mtiririko wa fedha ndani ya Shirika la Posta utaimarika pamoja na mizania ya Shirika kuruhusu upatikanaji wa mtaji kutoka kwenye Taasisi za Fedha kwa njia ya mikopo.

(c) Mheshimiwa Spika, huduma ya kutuma fedha hapa nchini ni huria na hakuna Taasisi yenye ukiritimba katika soko hilo. Mabenki pamoja na Taasisi nyingine za fedha hapa nchini pia hutoa huduma za utumiaji fedha. Kwa misingi hiyo hakuna sababu ya kuzungumzia ubinafsishaji wa huduma ya "*EMS Money Fax*" badala yake Serikali inachukua hatua muhimu za kuliwezesha Shirika letu la Posta ili litoe huduma ambayo ni bora zaidi na kwa ufanisi zaidi.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba huduma za Posta za *EMS* sasa hivi bado ni mbaya na kwamba Serikali inafanya jitihada ya kuziboresha huduma hizo. Je, isingekuwa busara wakati huu ambapo huduma hizi hazijaboreshwa gharama zake zikapunguzwa ili kulingana na huduma ambazo zinatolewa. Ahsante.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli gharama za usafirishaji kwa *EMS Money Fax* zinaonekana kwamba ni za gharama wakati huu. Lakini kama nilivyo Serikali iko mbioni ili kuhakikisha kwamba huduma hizi zinakuwa bora zaidi na zinatekelezwa kwa ufanisi zaidi, na hapo baadaye nitaeleza juu ya juhudi ya Serikali ya kujenga Mkonga wa Taifa wa mawasiliano yaani *ICT Backbone* ambao utarahisisha sana huduma hizi za mawasiliano na upelekaji wa vifurushi.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kutokana na swali la msingi kinachoonekana hapa ni kwamba kuna uzembe. Je, Serikali kama imejiandaa kuliimarisha Shirika hili, haioni kwamba ingeanza kushughulikia uzembe wa huduma iliyopo sasa hivi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, sikubaliani kwamba kuna uzembe katika huduma za Shirika la Posta. Nilichoeleza ni kwamba Shirika la Posta limekuwa na matatizo ya kifedha kiasi cha kwamba vituo vingine ambavyo vingeweza kutoa hiyo huduma vinashindwa kwa sababu ya kukosa fedha, na niseme tayari Serikali inachukua hatua ya kuchukua baadhi ya madeni na kufuta mengine ili Shirika liweze kujiendesha, na baada ya kufika katika hali hiyo. Shirika lina mipango tayari ili kusudi liweze kukopesheka na Taasisi za Fedha hapa nchini. Nina hakika tulipe muda hili Shirika na litaweza kufanya na kutoa huduma ambazo ni nzuri zaidi.

Na. 24

**Matatizo ya Mawasiliano Wilayani Kasulu**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna matatizo makubwa ya mawasiliano katika Wilaya ya Kasulu, hususani kwenye vijiji vya Kilelema na Heru- Ushingo vilivyopo mpakani mwa Tanzania na Burundi:-

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao ili kuwaondolea matatizo hayo kwa vile wanahitaji maendeleo ambayo yanaletwa kwa njia nyingi yakiwemo mawasiliano ya simu?

**SPIKA:** Mheshimwia Mbunge, ahsante sana, ni kweli ni swali namba 24.

**WAZIRI WA WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya awali juu ya utekelezaji wa mradi wa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano (*National ICT infrastructure Backbone*) pamoja na uanzishwaji wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*Universal Communication Access Fund for All – UCAF):-*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza sera ya Kitaifa ya *TEKNOHAMA* ya mwaka 2003 (*National ICT Policy* 2003), Serikali imeamua kujenga Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wenye uwezo wa kufikia Makao Makuu ya Mikoa yote na Wilaya zote – Tanzania Bara na Visiwani ifikapo Desemba, 2010 kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 170.

Mheshimiwa Spika, Mkonga huu wa Kitaifa utajengwa kwa teknolojia ya kisasa ya "*Fiber Optic*" kwa utaratibu wa mkopo wa masharti nafuu kutoka nchi rafiki ya Uchina. Mkonga huu utakuwa na uwezo mkubwa wa Kimataifa wa kubeba habari za aina zote ndani na sambamba kulenga kujiunganisha na mkonga wa baharini unaojulikana kama *Easy Cable*, *Seacom*, *UHURUNET* zitakazounganishwa katika Bandari ya Dar es Salaam as *landing site*). Mkonga wa Taifa utatumika katika utoaji wa huduma zote kama vile Serikali –Mtandao (*e-Government*), katika biashara (*e-business),* Elimu *(e-education*), afya (e- *medicine*), utalii (*e-tourism*) na kadhalika.

Aidha, itawezesha makampuni ya simu nchini kutoa huduma katika maeneo mengi zaidi katika nchi nzima na kwa gharama nafuu kwa watumiaji. Uwezeshaji huu

utachochea maendeleo ya wananchi kwa kasi kubwa zaidi. Mkonga wa Kitaifa wa Mawasiliano ukikamilika, utaendesha na vyombo vya Serikali. Kazi ya kuunganisha wateja kwenye mkonga na kusimamia matengenezo ya kila siku (*Operational Management of ICT Backbone*) yatafanywa na Kampuni yetu ya Simu ya *TTCL*.

Wakati Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa Mkonga wa Kitaifa wa Mawasiliano, pia inakamilisha taratibu za uanzishwaji wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*Universal Communication Access Fund for All*). Mfuko huu ulianzishwa kwa Sheria ya "*Universal Communication Access Act*" iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Novemba, 2006. Mfuko huu utawezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo magumu kibiashara, hususani vijijini, ambapo makampuni ya simu hayavutiwi kuwekeza kibiashara.

Mheshimiwa Spika, rasimu ya kanuni za Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote imechukua kipindi cha miezi 18 katika kuziandaa na kutafuta fedha za kuanzisha mfuko na zimekamilika Mei 2008. Hatua ya mwisho ni kuzitangaza kwenye gazeti la Serikali ifikapo Septemba, 2008 kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mfuko huu utaanza kutumika (*operationalisation*) ifikapo Desemba 2008. Aidha, Serikali ya Sweden kupitia Benki ya Dunia itachangia Dola za Kimarekani 30 milioni kwenye mfuko huu. Juhudi za kupata fedha hizi kupitia taratibu za Benki ya Dunia zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo huduma ya mawasiliano ya simu kwa wananchi Wilayani Kasulu pamoja na maeneo mengine nchini kwa lengo la kuwaongezea kasi ya maendeleo. Aidha, kwa kutambua umuhimu huo, Kampuni ya Simu ya *VODACOM* tayari imebaini maeneo husika hususan yale ya mipakani na mengine yenye shughuli za kibiashara kama vile katika vijiji vya Kilelema na Heru-Ushingo. Tathmini za kiufundi zitafanyika mwezi Agosti, 2008 ili kupata sehemu mahsusi kwa ajili ya kusimika mitambo ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *CELTEL* tayari imejenga minara katika maeneo ya Heru Juu Wilayani Kasulu na kufikisha huduma ya mawasiliano katika eneo hilo na maeneo jirani. Aidha, Kampuni hiyo bado inafanya utafiti wa masoko katika maeneo ya Kilelema na Heru-Ushingo ili kupeleka huduma za mawasiliano kwenye maeneo hayo ifikapo Desemba 2009.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kasulu, Kampuni ya *ZANTEL* inaendelea na awamu yake ya kwanza ya ujenzi wa minara ya mawasiliano na sehemu ambazo zimo katika awamu hii ni pamoja na Nyumbigwa, Kakonko na Muyasa na ujenzi huo utakamilika mwezi Septemba, 2008.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa tatizo lililopo Heru-Shingo pamoja na Kilelema ni sawa sawa na tatizo lililoko Mugambo na Kalia. Je, na wao ni lini watapata mawasiliano ya simu za mkononi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba Serikali imeona umuhimu wa kupeleka mawasiliano hadi kufikia vijijini na kwamba ujenzi wa mkonga wa mawasiliano ya Kitaifa utakuwa umekamilika kufika ngazi ya Makao Makuu ya Wilaya ifikapo mwaka 2010 na baada ya pale ule mfuko unaoanzishwa (*Universal Communication Access Fund for All - UCAF)* utasaidia kupeleka mawasiliano haya mpaka kufika vijijini. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba juhudi za Serikali ni kuwafikia wananchi walio wengi ili kusudi tuweze kuwa na mawasiliano mazuri. Siwezi kutamka kamili ni lini huduma hiyo itafika katika kijiji alichokitaja. Lakini nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wengi wanafikiwa na huduma hiyo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED**: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa mradi huu wa Serikali utawabebesha Watanzania deni kubwa sana. Na kwa kuwa yapo Makampuni ambayo tayari yameshawasilisha maombi yao ya teknolojia mpya kabisa ambayo ingerahisisha sana kuanza kuwapunguzia mzigo wa deni Serikali na wananchi. Lakini pili, wana teknolojia ya kisasa zaidi kuliko ya *fiber optic* ambayo Waziri ameitamka. Kwa nini Serikali kwa kuwa sasa inaruhusu watu binafsi kufanya biashara kwa nini wasiachie watu binafsi kufanya biashara badala yake Serikali inawabebesha Watanzania mzigo wa madeni bila ya sababu?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna Makampuni mengi ambayo yanataka kuwekeza hapa nchini ili kuweza kusaidia kasi ya maendeleo ya mawasiliano kwa wananchi. Tayari tukumbuke hapa nchini tayari tunayo mikonga ya Mashirika mbalimbali ikiwemo *TRA, TANESCO* na kadhalika.

Lakini nia ni kuunganisha nguvu zote hizi ili kusudi tusiwe na mikonga mbalimbali. Kwa sababu tunasema *we are talking about national optic fiber* lazima tuwe nao umoja. Nia ni kuunganisha hizi zote lakini kutakuwepo na *flexibility* ili kusudi wale wengine ambao wameshawekeza waweze ku-*recover* zile gharama zao.

Lakini kuhusu hizi Kampuni nyingine zinazokuja nafikiri sisi kama Watanzania vile vile tuwe waangalifu. Kuna matatizo ya kiteknolojia mambo ya *spectrum* ambayo vile vile yanafanyiwa kazi. Lakini vile vile kuna Makampuni ambayo yanataka kuingia hapa nchini kuchukua tayari mikonga ambayo tunayo.

Kwa mfano wa *TANESCO* ulitaka kuchukuliwa na Kenya na sisi tuko hapa. Hii mikonga inatumika vile vile kwa ajili ya usalama wa Taifa hili. Nafikiri lazima tuwe

waangalifu ili kusudi tusiruhusu kila mtu akaingia mpaka jimboni kwetu. Lakini pale ambapo taratibu ziko wazi Shirika letu litakuwa tayari kuruhusu Kampuni hizo nyingine.

Na. 26

**Migogoro ya Mgodi wa Buzwagi Kati ya Wananchi na Wawekezaji**

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi umekumbwa na migogoro kati ya wananchi na wawekezaji:-

(a) Je, tatizo ni nini?

(b) Je, Serikali imepanga kutatua mgogoro huo kwa kutumia njia gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi, umekuwa na migogoro kati ya wananchi na wawekezaji ambao chanzo chake ni tofauti za maoni ya viwango vya fidia na utaratibu uliotumika kuwahamishia wananchi kwenye makazi mbadala.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa tathmini ya kuwafidia na kuwahamisha wananchi waliokuwa wanaishi kwenye eneo la mradi ulianza mwaka 2005. Baada ya hatua za tathmini kukamilika wananchi wa vijiji vya Mwime, Mwendakulima na Chapulwa walilipwa fidia pamoja na kujengewa nyumba za makazi mbadala nyumba 205 kama mpango wa kuwafidia makazi yao ya zamani. Nyumba 207 zilitakiwa kujengwa.

Pia wachimbaji wadogo waliokuwa wanachimba kwenye leseni ndogo ya kijiji cha Mwime, eneo la Zanzibar na Majimaji wamefidiwa mashimo (maduara), maduara hayo 52 kila moja lilifidiwa shilingi 200,000.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na malipo hayo, migogoro iliendelea na mwezi Aprili mwaka huu 2008 yalitokea matukio ambayo yaliashiria kuhatarisha amani katika eneo hilo. Mheshimiwa Waziri Mkuu alimwagiza Waziri wa Nishati na Madini kushughulikia mgogoro huo ili kuupatia ufumbuzi. Tarehe 25 Aprili, 2008 Naibu Kamishna wa Madini alitumwa kufanya uchunguzi wa awali ili kumwezesha Waziri wa

Nishati na Madini ili kuushughulikia mgogoro huo. Baada ya taarifa ya Naibu Kamishna wa Madini kuwasilishwa kwa Waziri, Waziri alimtuma Naibu Waziri wa Nishati na Madini akiambatana na Kamishna wa Madini kwenda Buzwagi kutatua mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia tatizo hili:-

(i) Tulikutana na wahusika wote na kujadiliana kwa kina kuhusu kiini cha mgogoro. Hii ilijumuisha wawakillishi wa wananchi wa vijiji vyote vitatu yaani vijiji vya Mwendakulima, Chapulwa na Mwime, Mbunge wa Kahama Mheshimiwa Daudi Lembeli, Mkuu wa Wilaya na Uongozi wa Wilaya, na mwisho uongozi wa Mgodi *(Barrick*) ukiongozwa na Meneja wa *Barrick* Tanzania.

(ii) Baada ya kushauriana na wahusika wa pande zote tulifikia makubaliano ya kupitia upya masuala ya fidia kwa wananchi, ili kubaini kama kumekuwa na ukiukwaji wa namna yoyote. Tumejipa hadi tarehe 1Septemba, 2008 kupata majibu ya zoezi hili.

(iii) Aidha, masuala ya migogoro ya Barabara zinazounganisha vijiji, fidia za mialo (Marundo ya mchanga) na visima vya maji, na uboreshaji wa mawasiliano baina ya wananchi wanaozunguka mradi wa Mwekezaji, yamefikiwa makubaliano.

Mheshimiwa Spika, wananchi 14 walioshtakiwa Mahakamani kwa kosa la kushiriki kwenye mkusanyiko na maandamano yaliyozua vurugu katika geti kuu la mradi waliachiwa huru na Serikali, ili kuacha nafasi ya kushughulikia masuala ya fidia kwa uwazi, pia kuonyesha kuwa Serikali inataka kulimaliza suala hilo kiungwana ili wananchi na mradi waishi kama majirani wema kwa manufaa ya wananchi, mwekezaji na Taifa kwa ujumla.

Wananchi waliokataa kuhamia kwenye makazi mbadala mmojawapo akiwa Mzee Mashilimu Matunge Ngusa alitembelewa na Naibu Waziri wa Nishati na Madini na baada ya kubadilishana mawazo alikubali kuhama ili kupisha shughuli za ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji yaendelee. Mzee Mashilimu alikubali kuhama na akaomba ajengewe nyumba ya muda wakati nyumba ya kudumu inatayarishwa ili ahamie mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla sasa hali ni shwari na hatujapata taarifa ya matukio yoyote. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama, kwa ushirikiano mkubwa katika suala hili. Aidha, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge, kwa kujali maslahi ya wananchi hawa na haki zao.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na shukrani nyingi za dhati kwa kazi nzuri aliyoifanya alipotembelea Buzwagi kuona malalamiko, mahangaiko na matatizo ya wananchi hawa walikuwa wakiyapata, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa baada ya ziara ya Naibu Waziri huko Buzwagi wananchi na hususan wale ambao kaya 540 zilizohamishwa kutoka katika eneo la mgodi wanaendelea kuishi kwa matumaini kwa muda wa siku 90 ambazo Serikali iliahidi. Je, Serikali kupitia Bunge lako hili Tukufu, inaweza kwa mara nyingine kuwahakikishia wananchi hawa kwamba baada ya siku hizo 90 Serikali itatoa kauli yake kuhusu hatma ya mgogoro na matatizo ya wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru kwa ukarimu wa maneno yake lakini kazi tumeifanya kwa niaba ya wananchi wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, tulitoa ahadi ya siku 90 kwa sababu katika kufika pale tulibaini kwamba kweli kulikuwa na madai ya msingi kwa sababu tuliona kuna tofauti ambazo zilikuwa hazilingani. Kwa hiyo, tukafikia maamuzi ya kutoa siku 90 kwa sababu jambo lenyewe la fidia linahusisha watu wengi. Linahusisha Serikali za Wilaya, Serikali za Mkoa na linajumuisha pia sisi wenyewe kama Wizara. Lakini zaidi ya yote pamoja na uongozi wa *Barrick* Tanzania. *(Makofi)*

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Kahama kwamba kazi ya kupitia upya na kufanya tathmini sisi wenyewe kwa wenyewe tumeshaianza na matarajio yangu kwamba ndani ya siku hizo 90 tayari tunakuwa na majibu ya uhakika ya kuwafikisha wananchi wa maeneo hayo ya Kahama na kupitia ufumbuzi suala hili la fidia ya wananchi hao.

Na. 27

**Wilaya ya Kilwa Kupewa Mrahaba wa Mradi wa Songosongo**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kilwa iko nyuma kimaendeleo na ina hazina kubwa ya gesi asilia iliyoko kwenye Kisiwa cha Songosongo:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuipatia Wilaya hiyo mrahaba kutokana na mradi huo ili Wilaya iweze kutumia kifungu hicho kwa shughuli za maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Hakuna utaratibu wa kuzilipa moja kwa moja Halmashauri husika zinazozalisha gesi kama ilivyo kwenye Miradi mikubwa ya Madini, yenye mikataba *MDA's.* Utaratibu huu hauko kwenye Sera ya Nishati na hivyo mikataba iliyoingiwa na wawekezaji hao wa utafutaji wa gesi haikuweka utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dewji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hupata sehemu ya mauzo ya gesi ya asilia ya Songosongo na fedha hizo huwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, Hazina. Wilaya ya Kilwa kama Wilaya zingine nchini hupata mgao wake wa kugharamia shughuli za maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutoa fedha kwa ajili ya maendeleo ya Wilaya ya Kilwa, Serikali inatekeleza miradi sita kama jitihada za kuboresha maisha ya wakazi wa maeneo hayo ya Kilwa na maeneo yanayozunguka. Miradi hiyo ni pamoja na Mkuza wa bomba la gesi asilia ya Songosongo. Miradi hiyo ni pamoja na usambazaji umeme (*Wayleave Village Electrification Scheme – WVES).* Miradi mingine ni uchimbaji wa visima vya maji ambapo hadi sasa vimeshachimbwa visima 42 katika vijiji vilivyoko katika eneo la mradi pamoja na ujenzi wa kituo kipya cha kuzalisha umeme wa megawati 6 kutokana na gesi asilia ya Songosongo huko Somanga Fungu.

Vile vile kuna mradi wa ujenzi wa mfumo wa kusafirisha umeme wa kilovoti 33 kutoka Temeke hadi Mkuranga. Usambazaji umeme katika Wilaya za Kilwa na Rufiji unaendelea. Katika Kisiwa cha Songosongo usambazaji wa huduma mbalimbali kama vile maji ambapo lita 30,000 za maji husambazwa, umeme, upanuzi wa zahanati pamoja na ujenzi wa ghati umekamilika. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi pamoja na nyumba za kuishi askari Songosongo. Ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme na nyumba za wafanyakazi Somanga Fungu bado unaendelea.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya mkato ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya kumwuliza.

Si haki Kilwa kukosa mrahaba kutokana na gesi ya Songosongo. Je, Serikali haioni ibadili mikataba na Sera ya Umeme ili Kilwa, Mkuranga na *Mnazibay* kufanikiwa kupata mrahaba huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili nataka nijue kuhusu kusuasua kwa mradi wa Somanga Fungu mpaka leo Wilaya ya Kilwa na Rufiji haijapata umeme. Je, umefikia wapi umeme huo? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu katika swali la msingi nimetambua kwamba uzalishaji wa gesi haulipiwi mrahaba katika Wilaya husika.

Kama nilivyosema hili ni jambo ambalo limetokana na miongozi inayotolewa na Sera ya Nishati. Hata hivyo wakati tukiwasilisha Sheria ya Mafuta kama sehemu ya Sera ya Nishati, Wizara yangu ilisema hapa Bungeni kwamba tupo kwenye taratibu ya kubadilisha maeneo mbalimbali ndani ya Sera ya Nishati ambayo tunaona hayalingani na mfumo wa sasa wa kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, hivyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba masuala haya ya mrahaba wa gesi kama ilivyo wawekezaji wa maeneo ya madini yanazingatiwa na tunaangalia namna ya kuyaingiza ndani ya Sera ya Nishati na utekelezaji wake kwa ujumla hasa ikizingatiwa wananchi husika. Pia naomba niungane naye na mimi kama Mbunge wa Mkuranga pia ni mdau katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili linahusiana na mradi wa Somanga Fungu. Mradi wa Somanga Fungu ulikuwa ukamilike Julai, 2006. Kulikuwa na matatizo baina ya mkandarasi *G. P. Shapriya* na Wizara yetu. Lakini kwa kiasi kikubwa mkandarasi amekuwa anatoa ahadi ambazo hazikamiliki. Umeme huu kusema kweli kwa kukosekana kuchelewa mkandarasi anaathiri Wilaya ya Kilwa, Rufiji na Mkuranga pia.

Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba wiki iliyopita kabla hatujaja hapa Dodoma Ijumaa tulimwita mkandarasi *G. P. Shapriya* na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa William Ngeleja aliongea naye na akamtaarifu kwamba Serikali hatutokubali ucheleweshaji huu na kwamba tumempa ahadi mwisho wa mwezi wa nane ili akamilishe kazi hii na kama asipokamilisha kazi hii kusema kweli inabidi tuingie kwenye hatua nyingine kwa sababu ucheleweshaji wake unaathiri maendeleo ya wananchi wa Wilaya hizo.

Na. 28

**Elimu Juu ya Zao la Jatropha**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, zao la Jatropha linaweza kutupatia faida kubwa kwa kuongeza mapato ya Serikali na wananchi kuondokana na umaskini wa kipato; na kwa kuwa, hadi leo elimu juu ya zao hilo kwa wakulima bado ni ndogo:-

Je, Serikali ina mipango gani wa kuwapatia wakulima elimu zaidi na uhakika wa soko la zao hilo kwa Tanzania nzima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mafunzo juu ya zao hili la jatropha yametolewa kwa wataalam wa Ugani na wakulima katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Lindi, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam na Kilimanjaro.

Pamoja na mafunzo hayo ya moja kwa moja pia mafunzo kwa njia ya redio na vipeperushi yamekuwa yakitolewa wakati wote na kwa ukaribu na wadau wakati wa Sherehe za Nane Nane kwenye Kanda zote. Mkakati tulionao kwa sasa ni kuzalisha mbono kwa kushirikiana na wenye viwanda. Wakulima wanahamasishwa kuingia mkataba na kuzalisha kwa viwango vya muwekezaji.

Makampuni yaliyoandikishwa hapa nchini yanayonunua jatropha kwa sasa ni pamoja na Prokon ambayo ni Kampuni ya Kijerumani yenye Ofisi zake Mpanda Mkoa wa Rukwa na *Diligent* ya Kiholanzi yenye ofisi Arusha. Kilimo cha mkataba na wenye viwanda ndiyo njia pekee ya kuwahakikishia wakulima soko na bei nzuri.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo masuala mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mapema baada ya kujua umuhimu wa zao hili tuliweza kuwahamasisha wakulima kuanzisha zao hili kwa madhumuni ya kuondoa umaskini na kuongeza pato la Serikali na sasa hivi tayari wameshaanzisha kilimo hicho. Je, utakapofika wakati wa mavuno kule Visiwani Zanzibar ni utaratibu gani ambao utatumika ili wananchi wa kule kuweza kufaidika na mapato haya?

Swali la pili, kwa kuwa mazao ya biodizeli huwa yanaathiri mazao ya chakula. Je, Serikali imejiandaa vipi kuwapa elimu wakulima ili wasiathirike na balaa la njaa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema mwanzoni kwamba kilimo hiki cha jatropha ni bora kiwe kilimo cha mkataba.

Lakini kwa upande wa Zanzibar kwa sababu Wizara hii ya Kilimo sio ya Muungano, nadhani Wizara ya Kilimo kule Zanzibar itashughulikia suala hili.

Pili, mazao ya chakula kuhusu usalama wa chakula nchini. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini tayari imeshaunda kikundi kazi ambacho kinaandaa mwongozo na baadaye sera na baadaye itakuja kutunga sheria hiyo ya matumizi ya maeneo yetu kwa ajili ya jatropha ama mazao mengine yanayozalisha dizeli kwamba hususan jatropha na mazao mengine.

Sera hii na miongozo hii itatusaidia kubainisha maeneo ambayo yatalimwa mazao haya. Kwa sababu tunachoangalia hapa ni kulinda usalama wa chakula wa nchi yetu.

Lakini kwa sasa hivi ninachosema ni kwamba wananchi wasikubali kabisa kulima mazao haya ya jatropha maeneo ambayo yanalimwa mazao ya chakula.

Kwa mfano maeneo ya Iringa, Ruvuma, Rukwa na Mbeya maeneo ambayo tunajua kabisa yanatusaidia katika usalama wa chakula, maeneo haya kwa kweli si vyema na si bora kulima mazao ya jatropha ambayo yataharisha usalama wa chakula.

Pia wawekezaji wamekuwa wanahitaji mashamba makubwa sana yanayofikia hata hekta laki moja.

Sasa tunachowaomba wananchi wasikubali ni kuanza zile Serikali za Halmashauri kule kwenye Wilaya wasikubali kutoa maeneo makubwa kwa sababu tumeshasema kilimo cha mkataba kwa kutumia wakulima wadogo wadogo ndicho ambacho kingefaa zaidi. Maana wakichukua yale maeneo makubwa kwa kuwamilikisha itatuletea matatizo hapo baadaye ikizingatia kwamba bado tuna wajukuu. Bado tunazaa watoto wetu watakosa ardhi na hatutaki kufikia ile hali ya Zimbabwe ilifikia mahali pa kuwanyang'anya Wazungu. (*Makofi)*

Na. 29

**Kilimo cha Tumbaku Nchini**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, tarehe 29 Desemba, 2007 Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika alinukuliwa katika gazeti la Mtanzania akihutubia wananchi wa Kijiji cha Burega "B" Wilayani Tarime pamoja na mambo mengine kwamba, kilimo cha Tumbaku hakiruhusiwi Tanzania kutokana na ukosefu wa soko la uhakika:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya taarifa hiyo? Je, ni kweli Serikali imepiga marufuku kilimo cha Tumbaku?

(b) Kwa kuwa, Serikali inajua kuwa, wakulima wa Tumbaku hawana soko la uhakika na bei isiyoridhisha. Je, kwa nini imeshindwa kuwasaidia wakulima hao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Shughuli za sekta ndogo ya tumbaku nchini ikiwa ni pamoja na uzalishaji tumbaku mashambani huendeshwa kwa kuzingatia Sheria ya Sekta ya Tumbaku Na. 24 (2001) na Kanuni za Sekta ya Tumbaku za mwaka 2005. Kupitia Kanuni za Tumbaku kifungu cha 17(2) mikoa ambayo hadi sasa inaruhusiwa kuzalisha tumbaku kibiashara ni Tabora, Shinyanga, Singida, Rukwa, Mbeya, Iringa, Kigoma, Ruvuma, Lindi, Kagera, Tanga na Morogoro. Kwa hiyo kulingana na kanuni hizo, Mkoa wa Mara haumo katika mikoa iliyoruhusiwa kuzalisha zao la tumbaku nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haijawahi kupiga marufuku kilimo cha zao la Tumbaku nchini Tanzania kama ilivyonukuliwa na gazeti la Mtanzania. Nilichosema katika kijiji cha Burega B Wilayani Tarime ni kwamba kilimo cha zao la Tumbaku hakiruhusiwi katika Wilaya za Tarime na Serengeti kutokana na kukiukwa kwa Sheria ya Tumbaku. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Sheria Na. 24(2001) na kanuni za sekta ya Tumbaku za mwaka 2005, Mkurugenzi wa Kilimo hajaidhinisha Mkoa wa Mara kuwa miongoni mwa mikoa inayoruhusiwa kulima tumbaku kutokana na sababu zifuatazo:-

Hakuna ardhi ya kutosha Mkoa Mara kwa ajili ya kilimo cha tumbaku, kutokana na hitaji la kilimo cha kuhamahama kwa zao la tumbaku, kila baada ya miaka mitano.

Mkoa wa Mara hauna misitu mingi ya kukidhi mahitaji makubwa ya kuni kwa ajili ya kukaaushia tumbaku. Tumbaku iliyokuwa ikilimwa Mara ilikuwa ikisafirishwa kuuzwa Kenya, kinyume na Sheria ya Tumbaku inayopiga marufuku usafirishaji wa tumbaku mbichi nje ya nchi. *(Makofi)*

(b)Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa soko la tumbaku ya Tanzania tunapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tumbaku inayozalishwa Tanzania ina soko la uhakika kutokana na kiwango cha ubora wake.

Aidha, wasindikaji wa zao la tumbaku wamewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika ujenzi na ukarabati wa viwanda vya tumbaku. Wawekezaji hao wanatambua kwamba kama hakutakuwepo na zao la tumbaku kutoka kwa wakulima wa tumbaku nchini watapata hasara kubwa. Kutokana na hali hiyo, tumbaku yote inayozalishwa hununuliwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa maswali sasa unakaribia kikomo, kwa sababu tulianza na matangazo mengine, nitaruhusu dakika chache ili tuweze kuyamaliza maswali. Sasa swali la nyongeza, Mheshimiwa Said Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nimefarijika na taarifa hiyo na nimepata usahihi wa maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Nauliza hivi; zao la tumbaku ni zao ambalo linategemea sana mbolea toka hatua yake ya mwanzo ya kutayarishwa kwenye *seed bets* mpaka hatua ya mwisho. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mbolea ya ruzuku ya kutosheleza mahitaji halisi ya wakulima wa tumbaku katika zao la tumbaku na mazao ya chakula?

La pili, kwa kuwa tumbaku ni zao ambalo lina madaraja zaidi ya sitini na bei yake hatimaye unakuta kwamba imenunuliwa kwa chini au karibu ya nusu dola kwa kilo, kutokana na kuwepo kwa madaraja mengi. Hii haimsaidii mkulima wa tumbaku. Je, sasa Serikali ina mpango gani wa kuangalia kwamba mkulima huyu wa tumbaku ananufaika na bei inayotolewa na makampuni yanayonunua zao la tumbaku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme kwamba, kwa ujumla ruzuku inayotolewa na Serikali, haitaweza kutosheleza kwa sasa kwa mahitaji yote ya mbolea nchi nzima, kwa maana ya mazao ya chakula na biashara. Mahitaji kama nilivyosema hapo awali, *effective demand* ya mbolea nchini ni tani 385,000 na uwezo wa Serikali ni chini ya hapo; tani 100,000 ama tani 140,000.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu mbolea itaongezeka kidogo kutokana na mtakavyopitisha bajeti yetu ya Wizara ya Kilimo. Niseme kwamba, kilimo hiki cha tumbaku ni cha mkataba. Kwa hiyo, yale makampuni makubwa yanatoa *inputs* kwa maana ya mbolea, pamoja na dawa zinazohitajika. Lengo la Serikali hasa ni kutenganisha soko la pembejeo, pamoja na soko la tumbaku lenyewe.

Tunachotaka ni kwamba, Serikali iweze kulipa madeni yote ambayo vyama vile vya msingi vya tumbaku vinadaiwa kusudi wawe huru na vyama viwe huru, viweze kuchukua mbolea kutoka kwenye kampuni au shirika lolote; visifungwe na makampuni yale makubwa ambayo yananunua tumbaku. Tunataka tuwape uhuru huo na ndiyo

maana Serikali imekuwa inalipa madeni, kama tulivyoanza kwenye korosho na kwenye pamba, tunataka hata kwenye tumbaku madeni yale yanayodaiwa, ambayo yamehakikiwa yalipwe kusudi wakulima wale wawe huru. Tutofautishe *input market* na *output market*.

La pili, nadhani tukishatofautisha hayo mambo mawili, ili kuondoa mikono mizito ya yale makampuni, basi wananchi na vyama vyao, wataweza kupanga bei vizuri na kutakuwa na bei nzuri ya ushindani. (*Makofi*)

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nina swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko ya wakulima wa tumbaku kutokana na manunuzi ya zao la tumbaku kwa kutumia dola kwa biashara ya ndani ya zao; je, kwa nini Serikali kwa kushirikiana na wadau, isianzishe utaratibu wa kutumia Shilingi ya Tanzania ili kuondoa tatizo la kupunjwa pale ambapo dola inaanguka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Nkumba ni Mjumbe wa Bodi ya Tumbaku, kwa hiyo, kwa kushirikiana naye, tutaangalia ni vipi tunaweza kumnufaisha mkulima, aweze kupata fedha yake kwa kutumia sarafu iliyo nzuri. Ninakubaliana na yeye kwamba, kwa kutumia shilingi yetu na kuiheshimu ni bora kutumia Shilingi ya Tanzania kuliko kutumia fedha za nje.

Na. 29

**Biashara ya Mbao na Magogo**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa biashara ya mbao na magogo imekuwa na utata mkubwa na kuleta athari ya mazingira:-

(a) Je, Serikali inaendelea kutoa kibali kwa biashara hiyo na kama jibu ni ndiyo ni kwa vigezo gani na inadhibitiwa vipi?

(b) Je, kuna uwiano wa kitaalam kati ya uvunaji na utunzaji wa mazingira kwa maliasili hiyo?

(c) Je, Serikali inaweza kutoa utaratibu mzima ulio wazi wa utoaji wa leseni hadi kuvuna mbao/magogo vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inaendelea kutoa vibali kwa biashara ya mbao na magogo ili yachakatwe humu nchini, pale tu Wilaya husika itakapokuwa na Mpango wa Usimamizi wa Misitu ulioridhiwa na Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki. Aidha, Mpango huo unabainisha mahali uvunaji utakapofanyika, Mpango wa Upandaji Miti katika Wilaya, kiasi (ujazo) cha miti kitakachovunwa kila mwaka kwa muda wa miaka mitano, pamoja na kuorodhesha idadi ya viwanda vya mbao katika Wilaya. Hivyo, kila Afisa Misitu wa Wilaya, anatakiwa kuwa na Mpango wa Usimamizi wa Misitu.

(b) Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na ongezeko kubwa la mahitaji ya rasilimali ya misitu. Mahitaji haya yamesababisha uvunaji haramu na usio endelevu wa misitu na kuleta uwiano usio sawa kati ya uvunaji na upandaji miti. Wastani wa hekta 25,000 hupandwa kila mwaka, ikilinganishwa na kiwango cha hekta 91,276 za misitu zinazotoweka kwa mwaka. Serikali itahakikisha kuwa, kutakuwepo na uwiano kati ya uvunaji utakaoendana na utunzaji wa mazingira kwa maliasili hiyo. Hii ni kwa sababu uvunaji hautafanyika katika Wilaya yoyote ile, hadi hapo Wilaya itakapotayarisha Mpango wa Usimamizi wa Misitu. Aidha, ili mazingira ya kila Wilaya yaendelee kuboreshwa, kila mvunaji wa mazao ya misitu katika misitu ya asili, anatakiwa alipe asilimia tano ya ushuru wa mazao husika kwenye Mfuko Maalum, ambao fedha zake zinatumika kwa shughuli za kupanda miti na kuendeleza misitu. Aidha, Serikali kupitia miradi ya usimamizi shirikishi wa misitu, imesaidia kuweka misitu katika usimamizi madhubuti, chini ya Serikali za Vijiji na jumla ya hekta 2,060,000 zinasimamiwa na vijiji 1,102.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka 2006 ilitoa kitabu cha mwongozo wa uvunaji endelevu na biashara ya mazao ya misitu. Mwongozo huu, unaweka utaratibu madhubuti utakaofuatwa katika uvunaji na biashara ya mazao ya misitu ili kudhibiti uvunaji usio endelevu. Utaratibu ni kama ufuatao:-

- Kupata barua yenye idhini ya Serikali ya Kijiji na kujadiliwa katika Kamati za Uvunaji za Wilaya.
- Mwombaji atakayechaguliwa inabidi ajisajili kufanya biashara ya mazao ya misitu kwa Mshauri wa Maliasili wa Mkoa.

- Baada ya kujisajili atapewa leseni ya uvunaji na Afisa Misitu wa Wilaya.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri; anaweza akatupatia kama Wabunge, nakala ya mwongozo anaouzungumzia ili tuweze kufuatilia kwa karibu nini kinachotendeka katika Wilaya zetu?

La pili, ni Makampuni gani hayo ambayo bado mnatoa vibali ili waendelee na biashara hiyo na katika makampuni hayo; yapo ambayo yapo katika Wilaya yangu ya Liwale?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu maswali ya Mheshimiwa Kigwalilo na kutokana na kuguswa na maswali yake, ninaomba nimshukuru sana na kumpongeza kwa jinsi anavyotushauri na kutusaidia katika Wizara, lakini pia kwa jinsi ambavyo amekuwa akishirikiana na wananchi wake, kupenda ku-*achieve maximum results* kutokana na rasilimali za maliasili zilizoko kwenye Wilaya yake.

Mheshimiwa Spika, niseme tu nimempongeza Mheshimiwa Kigwalilo, kwa sababu katika hii mipango ya uvunaji wa rasilimali za misitu katika Wilaya zote, kwenye nchi yetu ni Wilaya 11 ambazo zimeshaandaa mpango huo na Wilaya ya Liwale imo; na kwa mwaka huu wa fedha wamepanga kuvuna karibu miti yenye ujazo wa 1,090,000 na watapata karibu milioni 100 kutokana na mpango wao waliojiwekea, ambao Mkurugenzi wa Misitu ameshaidhinisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kigwalilo, nampongeza na Wilaya yake.

Kwa swali lake la kwanza; nakubali kwamba mwongozo huu tutaugawa na nitawasiliana na wenzangu Ofisini kuhakikisha tunaugawa kwa Wabunge wote mapema iwezekanavyo na yawezekana ndani ya wiki zisizozidi mbili.

Kwa swali la pili; Makampuni yanayofanya biashara ya mazao ya misitu yapo mengi. *Licensing* ya biashara ya misitu inafanyika kwenye Wilaya, kama nilivyosema kwamba, Kamati za Ugawaji za kila Wilaya, zinatoa Leseni ya mtu kuangusha au ku-*fell timber*. Kwa hiyo, yapo makampuni mengi yaliyotapakaa nchi nzima. Lakini kwa makampuni ambayo yana-*export* mazao ya misitu, yaani mbao, kwa sasa hivi yapo machache na hayazidi matano na ni kampuni moja tu ambayo inafanya kazi kwenye Wilaya ya Kilwa, inaitwa *Mtui Sawmills* na yapo makampuni madogo madogo ya wakazi wa Wilaya hiyo wasiozidi 11.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali na majibu umepita na maswali yamekwisha, sasa ni matangazo machache.

Napenda nitambue na Waheshimiwa Wabunge mtambue, uwepo wa *IGP*, Mheshimiwa Said Mwema, akisindikizwa na *RPC* wa Dodoma, Omar Mganga. (*Makofi*)

Naomba pia mtambue uwepo wa Mwenyekiti wa *CUF* Taifa, Mheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba, amefuatana na Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi wa Taifa la *CUF*, ambao ni Mheshimiwa Said Miraji na Mheshimiwa Dr. Juma Muchi; karibuni sana. (*Makofi*)

Ninao wageni wangu kutoka Mkoani Tabora; ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi ya Mkoa. Samahani, Mheshimiwa *IGP* Mwema alitoka kidogo, karibu sana Mheshimiwa Mwema na tunaendelea kuwa na imani nawe, kwa kazi kubwa sana mnayoifanya ya kupambana na uhalifu kwa ukaribu sana. (*Makofi*)

Wageni wangu hao wapo 15, lakini wanaongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Hassan Wakasuvi, Katibu wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Asha Kipangula na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Abeid Mwinyimsa. Karibuni sana, tunafurahi kuwaona hapa na nampongeza sana Katibu wa CCM Mkoa wa Tabora, kwa utaratibu alioufanya wa kuweza kuwaleta Wajumbe wote wa Kamati ya Siasa, kuja hapa kushuhudia Bunge. Tunaomba Mikoa mingine nayo, iige mambo mazuri mazuri kama haya. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wa Mheshimiwa Mtutura, Mbunge wa Tunduru; yupo baba yake mzazi, Mzee Alai Rashid Mtutura, karibu sana na pole sana na safari ndefu kutoka Tunduru. Yupo pia Mzee Daimu Kalonga na kijana aliyefuatana na Wazee hawa, ambaye ni Sunday Seif Litapa; wale pale. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Ernest Mabina ni Isaka Wandiba na Iman Abdallah wale pale. Hawa ni Wenyeviti wa katika Kijiji cha Mugusu. Mmoja ni Mwenyekiti wa Kijiji na mwingine ni Mwenyekiti wa CCM wa Tawi.

Wageni wa Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula ni binti yake Somoe Mayawe, yule pale na mume wa Binti huyo, ambaye ni George Mayawe. Ninaona kuna mtoto mchanga, basi nadhani tumpongeze Mheshimiwa Tatu Ntimizi kwa kupata mjukuu. (*Makofi*)

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa N Dr. Lucy Nkya, anao wageni wake nadhani watakuwa wanatoka Morogoro; nao ni Mama Mnai, Petro Nkya na Aman Mnai, wale pale kiribuni sana.

Ndani ya Ukumbi pia katika *galleries* sijui ni wapi; tunao Waheshimiwa Wabunge Wastaafu; Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Christopher Wegga yule pale. Natumaini ninyi niliowaita wastaafu, mmekuja kwa nia njema tu kushuhudia Bajeti. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu vikao; Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Ndugu Anselem Mrema, anawaomba Wajumbe wa Kamati za Huduma za Jamii, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na Kamati ya Miundombinu kwamba, kamati hizo nne wakutane kesho tarehe 13 Juni, 2008 saa tatu asubuhi katika Ukumbi unaoitwa African Dream, Mlimwa - Area D hapa Dodoma. Semina hiyo imeandaliwa chini ya Mradi wa *Deepening Democracy* na Itifaki zote za Semina zimezingatiwa.

Mheshimiwa Ali Ameir, Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM, anaomba Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, wakutane katika kikao kifupi sana cha dharura leo mara tu baada ya kusitishwa shughuli za asubuhi.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wakutane kesho saa nne asubuhi Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo, mkutane kesho saa nne asubuhi; hakutaja Ukumbi lakini nadhani itakuwa kwenye Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, natoa rai kwa Waheshimiwa Mawaziri kwamba, kutakuwa na uhamisho mdogo; kutokana na madabiliko mbalimbali na kwa sababu mipangilio ya kuwapanga Mawaziri inafuata *seniority*, inabidi Katibu afanye mabadiliko madogo. Huu ni utaratibu wa kawaida tu, lakini natangulia kusema hivyo, kwa sababu mtasogeasogea kidogo ili kuzingatia utaratibu.

Mheshimiwa Mwijage, amelalamika kwamba, sijatangaza wageni wake, lakini sijaona katika karatasi labda ilikuwa imesahauliwa. Naomba mgeni wa Mheshimiwa Mwijage asimame; ni mmoja tu, ahsante sana.

Wakati natangaza Mheshimiwa Balozi wa Uingereza ameingia hapa ndani na si Balozi ila ni Mgeni kutoka Ubalozi wa Uingereza. *We have a problem; is that High Commissioner? No, anyway our guest from the British High Commission in Dar es Salaam*. Hapana? Sasa mbona mmeniandikia hapa? Basi nitaliacha hilo litanichukulia muda, natumaini anaweza kuwepo jioni tutarekebisha hali. Kwa sasa nimwite Katibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2007 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2008/2009

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2007 na Mwelekeo katika Muda wa Kati - 2008/09 – 2010/11). Pamoja na Hotuba hii, nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2007 na Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru sana, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshima Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa maoni na ushauri mzuri wakati wa kujadili muhtasari wa taarifa hii. Kamati hii imetoa mchango mkubwa katika kuboresha taarifa ya hali ya uchumi na mapendekezo ya sera za jumla za uchumi na mwelekeo wa Bajeti ya Serikali ya 2008/09.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu kwa Naibu Mawaziri wa Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, Katibu

Mkuu, Ndugu Gray S. Mgonja, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango, Balozi Charles K. Mutalemwa, Naibu Makatibu Wakuu; Ndugu Ramadhani M. Khijjah, Ndugu John M. Haule na Ndugu Laston T. Msongole, Makamishna, Wakurugenzi, Viongozi wa Asasi zilizo chini ya Wizara na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, ambao wamefanya kazi kubwa ya kuandaa taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Viongozi na Wafanyakazi wenzetu wa Wizara, Mikoa, Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma, kwa ushirikiano wao wakati wa kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, shukrani za dhati nazitoa kwa wapiga kura wangu, Wananchi wa Jimbo la Kilosa, kwa kunichagua kuwa Mbunge wao. Ninachoweza kusema hapa ni kuwaahidi kwamba, sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kwa heshima kumpongeza, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa kwa kishindo na Bunge lako Tukufu. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, walioteuliwa na Mheshimiwa Rais mwaka huu wa fedha. Napenda vilevile kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, walioteuliwa na Mheshimiwa Rais; Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Dr. Christine Gabriel Ishengoma na Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir. Nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, kwa kushinda katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Kuchaguliwa kwa Mheshimiwa Rais, kunazidi kuiweka nchi yetu juu zaidi katika medani za Kimataifa. Mtakubaliana nami Waheshimiwa Wabunge kwamba, hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu. Aidha, nakupongeza sana wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuteuliwa kwako kuwa Makamu wa Rais wa Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola (*CPA*). Uteuzi huu unazidi kuipa heshima nchi yetu juu ya uwezo wa Watanzania katika uongozi Kimataifa. Tunakutakia kila la heri katika kutekeleza jukumu hilo kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imepata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nane wa Leon Sullivan, uliofanyika Mkoani Arusha tarehe 2 - 6 mwezi huu wa Juni, 2008. Mkutano huu wenye lengo la kuwakutanisha Waafrika na Wamarekani wenye asili ya Afrika, kujadili fursa za maendeleo, ulihudhuriwa na watu zaidi ya elfu nne na ulikuwa wa mafanikio makubwa. Ni mategemeo ya Serikali ya Tanzania kuwa, wafanyabiashara, wawekezaji na watalii wengi zaidi wa Marekani waliohudhuria, hata wale wasiohudhuria mkutano huu, watarudi kuwekeza, kufanya biashara na kutalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na familia za Waheshimiwa Wabunge wenzetu, waliotangulia mbele ya haki katika kipindi hiki cha mwaka mmoja. Marehemu Salome Mbatia, ambaye alikuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na

Watoto na Marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, shabaha na malengo ya uchumi jumla katika mwaka 2007/08 -2009/10: Kabla ya kutoa taarifa ya hali ya uchumi kwa mwaka 2007 na mwelekeo wa muda wa kati, naomba kuelezea misingi na shabaha kuu za kisera katika kipindi cha 2007/08 -2009/10. Tangu mwaka 1999, Sera na Mipango ya maendeleo ya Nchi yetu, imelenga katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa hadi mwaka 2025. Dhana ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, inatokana na mtazamo wa jamii unaotaka kumkomboa Mtanzania kiuchumi na kijamii. Aidha, Dira ya Maendeleo ni kielelezo cha mtazamo wa Taifa katika kufanikisha matakwa au matumaini ya kuwa na maisha bora kwa kila mwananchi katika muda uliokusudiwa. Dhana hii ya Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, ndiyo msingi mkuu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, Dira ya Maendeleo ndiyo inayoongoza mwelekeo wa Sera za Uchumi na Maendeleo ya Wananchi hadi 2025. Dhamira kuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ni Tanzania kuweza kujinasua kutoka katika nchi yenye viwango vya chini vya maendeleo hadi kufikia viwango vya maendeleo vya kati. Ili kufikia malengo ya Dira 2025, Serikali imebuni na kutekeleza Mikakati, Mipango na Programu mbalimbali, ambazo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Mipango ya Muda wa Kati *(Medium Term Plans);*

(ii) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA);

(iii) Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania 2020 – *Mini Tiger Plan 2020;*

(iv) Malengo ya Maendeleo ya Milenia – *Millennium Development Goals;*

(v) Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania – MKUMBITA;

(vi) Programu za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF);*

(vii) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania – MKURABITA;

(viii) Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na

(ix) Mikakati na Programu za Kisekta.

Aidha, mikakati na mipango hii, imejumuishwa katika Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007, mfumo wa takwimu za Pato la Taifa Tanzania Bara, ulifanyiwa marekebisho yaliyolenga kuimarisha ubora wa takwimu hizo ili ziweze kutoa picha halisi ya shughuli za kiuchumi nchini na kulinganishwa kimataifa, kama ilivyoainishwa katika mfumo wa takwimu za Pato la Taifa wa Umoja wa Mataifa. Mwaka wa ulinganisho wa takwimu za Taifa sasa ni 2001, badala ya 1992 uliokuwa unatumika awali.

Mheshimiwa Spika, historia ya kutayarisha takwimu za Pato la Taifa Tanzania Bara, ilianza mwaka 1954. Tangu wakati huo, maboresho yamekuwa yakifanyika mara kwa mara pale ilipolazimu kufanya hivyo, kulingana na taswira halisi ya uchumi wetu. Aidha, vigezo muhimu vilivyotumika kutayarisha takwimu za Pato la Taifa kwa miaka ya nyuma, vilizingatia zaidi dhana na mifumo ya takwimu za Pato la Taifa ya Umoja wa Mataifa ya miaka ya 1953, 1968 na 1993. Marekebisho ya kwanza ya takwimu za Pato la Taifa, yalifanyika kwa kutumia bei za mwaka 1966. Makisio ambayo yalitumia mfumo wa takwimu za Pato la Taifa wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1953.

Marekebisho ya pili, yalifanyika kwa kutumia bei za mwaka 1976, kulingana na mfumo wa takwimu za Pato la Taifa wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1968. Marekebisho ya tatu, yalifanyika kwa kutumia bei za mwaka 1992, makisio ambayo yalitumia mfumo wa takwimu za Pato la Taifa wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1968 na sehemu ndogo ya mfumo wa mwaka 1993. Mheshimiwa Spika, marekebisho ya sasa ya takwimu za Pato la Taifa, yametumia bei za mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, sababu za kuchagua 2001 kuwa mwaka wa kizio ni kwa kuwa mwaka huo ulikuwa na takwimu za kutosha toka vyanzo mbalimbali, ambazo hazikuwahi kujumuishwa katika mfumo uliopita wa takwimu za Pato la Taifa. Marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa, yalikuwa pamoja na kukadiria makisio ya mwaka wa kizio na miaka iliyopita, mwaka wa kizio na miaka inayofuata. Marekebisho ya mwaka wa kizio na makisio ya takwimu za Pato la Taifa, yalitokana hasa na sababu zifuatazo:-

(i) Takwimu zilizokuwepo kwa bei za mwaka 1992 zilikuwa zimepitwa na wakati na hazikuwa zikionyesha mabadiliko halisi ya muundo wa uchumi uliokuwa umetokea nchini tangu wakati huo;

(ii) Umuhimu wa kutambua mabadiliko ya muundo wa uchumi, hususan katika uzalishaji, matumizi na uwekezaji;

(iii) Kuzingatia katika Takwimu za Taifa, mabadiliko ya mahusiano ya bei za bidhaa mbalimbali yaliyojitokeza ndani ya kipindi hicho;

(iv) Kuboresha orodha ya bidhaa na huduma sanjari na ubunifu unaoleta thamani kubwa ya bidhaa na huduma mbalimbali mpya katika soko;

(v) Kujumuisha taarifa na takwimu zote mpya katika shughuli mbalimbali za uchumi kutokana na tafiti mpya zinazofanyika kama vile Tafiti za Matumizi ya Kaya Binafsi; na

(vi) Kujumuisha mahitaji na maelekezo mapya kulingana na mfumo wa kimataifa wa takwimu za Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia marekebisho hayo, mfumo wa uchumi wa Tanzania, umewekwa katika maeneo makuu manne ya kiuchumi, badala ya sekta tisa kama ilivyokuwa awali. Maeneo hayo makuu ni (i) Kilimo, Uwindaji na Misitu (ii) Uvuvi (iii) Viwanda na Ujenzi na (iv) Huduma.

Mheshimiwa Spika, aidha, mabadiliko hayo ya ulinganisho wa takwimu kwa kutumia kizio cha mwaka 2001, yamebadili muundo na mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa. Shughuli za kilimo zilikuwa na mchango wa asilimia 44.7 katika Pato la Taifa, kwa kutumia kizio cha mwaka 1992. Kwa kutumia kizio cha 2001, kilimo kimechangia asilimia 25.8 mwaka 2007, ikiwa na maana kwamba, mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa umepungua, kwa sababu sekta nyingine zimekua kwa kasi kubwa kuliko kilimo na pia takwimu zinazotumika kukokotoa mchango wa kila sekta, zinazingatia gharama za mwaka husika na ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007, Pato Halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 7.1, ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2006. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na sekta za mawasiliano (asilimia 20.1), madini (asilimia 10.7), huduma za fedha (asilimia 10.2), biashara (asilimia 9.8), ujenzi (asilimia 9.7), afya (asilimia 8.8) na kilimo kilikua kwa asilimia 4.0.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa Pato la Taifa kutoka shilingi milioni 17,941,268 mwaka 2006 hadi shilingi milioni 20,948,403 mwaka 2007 na tukizingatia kwamba, idadi ya watu Tanzania Bara ni takriban watu milioni 38.2, Pato la Wastani la Mtanzania limefikia shilingi 548,388 kwa mwaka, ikilinganishwa na shilingi 478,434 mwaka 2006; ongezeko la asilimia 14.6.

Maelezo ya takwimu hii ni kwamba, kama Pato la Taifa la shilingi trilioni 20.9 mwaka 2007 lingegawanywa kwa usawa kwa kila mwananchi, basi kila mtu angepata shilingi 548,388 kwa mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007, uchumi wa Taifa, kama zilivyokuwa chumi nyingine duniani, ulikumbwa na unaendelea kukumbwa na misukosuko ya kupanda kwa fahirisi ya bei za bidhaa na huduma, kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli na bei za vyakula katika soko la dunia. Kasi ya upandaji wa bei ilikuwa wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka ulioishia 2007.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa mwezi Aprili 2008, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 9.7, kutoka asilimia 7.0 mwezi Disemba, 2007. Kiwango hicho kinatarajiwa kushuka, kutokana na msimu wa mavuno ya chakula, ambao umeanza katika

baadhi ya maeneo ya nchi. Hata hivyo, mfumuko wa bei nchini, utaendelea kuwa zaidi ya asilimia tano, ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuendelea kupanda kwa bei za mafuta ya petroli katika Soko la Dunia. Serikali inachukua hatua za kuhakikisha chakula cha kutosha kinazalishwa hapa nchini. Maelezo ya kina ya hatua hizo yatatolewa na Waziri anayesimamia sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007, ukuzaji rasilimali uliongezeka na kufikia shilingi 6,209,741 milioni, kutoka shilingi 4,957,781 milioni mwaka 2006, kwa bei za miaka hiyo, sawa na ongezeko la asilimia 25.3. Thamani hiyo ya rasilimali ni asilimia 29.6 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na asilimia 27.6 mwaka 2006. Ongezeko hilo la ukuzaji rasilimali limetokana hasa na ongezeko katika ujenzi wa majengo, uingizaji kutoka nje mitambo na vifaa vya uwekezaji, uendelezaji ardhi, barabara, madaraja na shughuli nyingine za uchumi na biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa kalenda wa 2007, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana *($M_2$)1* uliongezeka kwa asilimia 28.8 ikilinganishwa na asilimia 13.7 mwaka 2006. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi *($M_3$)*, uliongezeka kwa asilimia 21.4 mwaka 2007, ukilinganishwa na asilimia 22.0 mwaka 2006. Ongezeko la $M_2$ lilichangiwa na kuongezeka kwa amana za hundi, kufuatia ongezeko kubwa la mikopo ya benki kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa kalenda 2007, mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 42.2, ikilinganishwa na lengo la asilimia 34.8. Mikopo iliongezeka kutoka shilingi milioni 2,028,294.3 Disemba, 2006 hadi shilingi 2,883,789.5 milioni Disemba, 2007. Mikopo mingi ilielekezwa katika sekta za viwanda (asilimia 19.3); biashara (asilimia 17.2); kilimo (asilimia 9.9); na usafirishaji na mawasiliano (asilimia 7.0). Ongezeko hili la mikopo ya benki limechangiwa na kuongezeka kwa ushindani katika sekta ndogo ya benki na mwamko wa wananchi kutumia huduma za benki.

Mheshimiwa Spika, riba za dhamana au hatifungani za Serikali, zilishuka kutoka wastani wa asilimia 17.1 mwezi Juni, 2007 hadi asilimia 11.4 mwisho wa Disemba, 2007. Aidha, riba ya mikopo ya benki za biashara, ilishuka kutoka wastani wa asilimia 16.0 mwisho wa mwezi Juni, 2007 hadi asilimia 15.1 mwezi Machi, 2008. Kushuka kwa riba ya hatifungani za Serikali ni matokeo ya Serikali kusitisha kukopa kutoka kwenye soko la ndani la fedha kwa ajili ya matumizi yake na hatua madhubuti zilizochukuliwa na Benki Kuu, kusimamia soko la dhamana za Serikali na lile la fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa lilipungua kidogo kutoka Dola za Marekani milioni 7,188.4 Disemba, 2006, hadi Dola milioni 7,041.2 Disemba, 2007. Dola milioni 1,673.5 ni deni la ndani, sawa na asilimia 23.8 ya deni lote na deni la nje ni Dola milioni 5,367.7. Sehemu kubwa ya deni la ndani ni dhamana za Serikali zilizouzwa katika soko la dhamana. Kupungua kwa Deni la Taifa kulitokana na msamaha wa madeni ya nje chini ya Mpango wa *HIPC1 Debt Relief* na mpango wa kufutiwa madeni yanayodaiwa na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa (MDRI).

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mwenendo wa sekta ya nje si wakuridhisha sana, kutokana na kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara ya nje kutoka dola za Marekani milioni 1,379.3 mwaka 2006 hadi Dola milioni 2,056 mwaka 2007 (ongezeko la asilimia 49.1). Nakisi hiyo imechangiwa zaidi na kasi kubwa ya ongezeko la thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje, ikilinganishwa na thamani ya bidhaa na huduma zilizouzwa nje ya nchi. Aidha, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya Dola milioni 4,826 mwaka 2007 kutoka Dola milioni 3,864.1, imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli, pamoja na ongezeko la uagizaji mitambo na malighafi.

Hata hivyo, thamani ya mauzo ya huduma kama vile utalii, biashara na usafirishaji nje, hasa kutoka Dar es Salaam kwenda katika nchi za jirani, imekua kwa kasi ya kutia moyo mwaka 2007. Kwa hali hii Serikali itaongeza nguvu katika kuweka mazingira mazuri zaidi ya kukuza mauzo ya bidhaa na huduma nje kwa kuwa hii ni njia muhimu ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, wastani wa thamani ya sarafu ya Tanzania ikilinganishwa na sarafu ya Kimarekani kwa mwaka 2007, ilikuwa ni wastani wa shilingi 1,244.1 kwa Dola moja, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,253.9 kwa Dola moja mwaka 2006. Aidha, thamani ya sarafu ya Tanzania mwisho wa Disemba, 2007 ilikuwa shilingi 1,132.1 kwa Dola moja, ikilinganishwa na shilingi 1,261.6 mwisho wa Disemba, 2006. Kupanda kwa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Marekani, kulitokana na kushuka kwa nguvu ya Dola dhidi ya fedha za nchi tajiri tunazofanya nazo biashara na maboresho katika uendeshaji wa soko la dhamana za Serikali katika Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na urari wa malipo ya nje kuwa na nakisi, mwaka 2007 akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kwa asilimia 21.9 na kufikia Dola milioni 2,755.2, kutoka Dola milioni 2,260.1 mwaka 2006. Akiba hii ya fedha za kigeni, ilikuwa inatosha kulipia bidhaa na huduma zinazoagizwa kutoka nje kwa miezi 4.6.

Mheshimiwa Spika, viashiria mbalimbali vinaonyesha kwamba, hali ya uchumi duniani sio imara. Uko upungufu mkubwa wa chakula kutokana na kupungua kwa uzalishaji, kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa na pia nchi tajiri kutumia nafaka kwa wingi kuzalisha nishati. Matokeo yake ni kupanda kwa bei ya chakula duniani kote. Aidha, sekta ya fedha katika masoko ya kimataifa, nayo inayumba kutokana na wateja wa benki kushindwa kurejesha mikopo ya nyumba. Mabadiliko ya hali ya hewa pia yanaathiri chumi za nchi zote duniani, ingawa viwango vya athari vinatofautiana. Bei ya mafuta ya petroli, vifaa vya ujenzi kama saruji, malighafi za viwanda na pembejeo za kilimo hasa mbolea, imeendelea kupanda. Kutokana na sababu hizi na nyingine kama ukosefu wa amani katika maeneo kadhaa duniani, taarifa zinaonyesha kwamba, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2007, kulinganisha na wastani wa ukuaji wa asilimia 5.3 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya ukuaji wa uchumi wa dunia mwaka 2008/09 sio ya kuridhisha kutokana na kuendelea kuvurugika kwa masoko ya fedha ya kimataifa, kutokana hasa na vurugu za soko la nyumba nchini Marekani na Ulaya ya Magharibi,

pamoja na kupungua kwa upatikanaji wa mikopo mipya ya nyumba. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia, haitegemewi kuzidi wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2008, isipokuwa chumi za China na India ambazo zimeendelea kukua kwa viwango vya asilimia 11.4 (China) na 9.2 (India) mwaka 2007. Mwenendo huu wa hali ya uchumi wa dunia, unahofiwa kuathiri uwekezaji katika nchi zinazoendelea *(FDI)* na hivyo nchi hizo kushindwa kukua kwa kasi inayohitajika kupunguza umaskini na kushindwa kufikia malengo ya Milenia. Aidha, upo uwezekano wa nchi hizo kushindwa kukabiliana na mfumuko wa bei kutokana na kuendelea kupanda kwa bei za mafuta ya petroli, vyakula, pembejeo za kilimo na malighafi za viwanda. Kwa hali hii, hatuna budi kujizatiti kukabiliana na changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007, Pato la Bara la Afrika lilikua kwa wastani wa asilimia 6.2, ikilinganishwa na asilimia 5.9 mwaka 2006. Pato la nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, liliongezeka kutoka asilimia 6.4 mwaka 2006 hadi asilimia 6.8 mwaka 2007. Ongezeko hilo lilitokana hasa na ukuaji mkubwa wa pato kwa nchi zinazouza mafuta ya petroli hasa Angola na Nigeria na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kwa nchi nyingine kadhaa za Afrika. Mwaka 2007, uchumi wa Angola ulikua kwa asilimia 21.1, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji na bei ya mafuta na almasi. Ukiondoa nchi zenye mafuta ya petroli, Tanzania ni moja ya nchi zilizokuza Uchumi kwa kiwango kikubwa katika Bara la Afrika Kusini mwa Sahara.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa sekta mbalimbali wataeleza kwa kina, maendeleo katika maeneo yao na hivyo katika hotuba hii, nitatoa tathmini ya kijumla tu ya maendeleo katika baadhi ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kilimo, mifugo, misitu na uwindaji, zilikua kwa asilimia 4.01, mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2006. Ukuaji huu ulitokana hasa na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji wa mazao kutoka asilimia 4.0 mwaka 2006 hadi asilimia 4.5 mwaka 2007. Aidha, ukuaji wa shughuli za mifugo na mazao yake ulikuwa asilimia 2.4 mwaka 2007, sawa na ilivyokuwa mwaka 2006. Ukuaji katika shughuli za misitu na uwindaji ulishuka kutoka asilimia 4.6 mwaka 2006 hadi asilimia 2.9 mwaka 2007, kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya misitu, kwa sababu ya kusitishwa kwa muda kwa usafirishaji holela wa magogo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008/09 vipaumbele vya Serikali katika shughuli za kilito, vitaelekezwa katika uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji; utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)*, ambayo ni pamoja na kutumia mbegu bora, kuongeza matumizi ya mbolea; na kuibua masoko ya mazao ya kilimo. Aidha, mkazo utawekwa katika ukarabati wa barabara za vijijini na kuzihuisha upya leseni za misitu na uwindaji.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uvuvi zilikua kwa kiwango cha asilimia 4.5 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2006. Kasi hii ndogo ya kukua kwa uvuvi imetokana hasa na kuendelea kwa vitendo vya uvuvi haramu; kupungua kwa mahitaji ya samaki na mazao yake katika masoko ya nje; uharibifu wa mazingira katika mazalia ya samaki; na matumizi ya zana duni za uvuvi. Upo uwezekano pia wa hujuma

katika biashara ya samaki. Mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 1.3 mwaka 2007, kama ilivyokuwa katika mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Serikali itaweka mkazo katika kudhibiti uvuvi haramu na kuhifadhi mazingira katika maeneo tengefu. Serikali pia inafanya upembuzi yakinifu, kwa lengo la kuongeza mchango wa uvuvi katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, katika mgawanyo mpya wa takwimu za Pato la Taifa, shughuli za viwanda na ujenzi zinajumuisha uzalishaji bidhaa viwandani, umeme, gesi, usambazaji wa maji, madini, uchimbaji wa mawe, na ujenzi. Shughuli za kiuchumi katika viwanda na ujenzi, ziliongezeka kwa kiwango cha asilimia 9.5 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2006.

Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji kulichangiwa na kukua kwa uzalishaji bidhaa viwandani, umeme na gesi, usambazaji maji na ujenzi. Hata hivyo, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika madini na uchimbaji mawe, kilipungua kutoka asilimia 15.6 mwaka 2006 hadi asilimia 10.7 mwaka 2007. Mchango wa shughuli za kiuchumi za viwanda na ujenzi katika Pato la Taifa, uliongezeka na kufikia asilimia 21.2 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 20.8 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani zilikua kwa kiwango cha asilimia 8.7 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2006 na zilichangia asilimia 7.8 ya Pato la Taifa mwaka 2007, sawa na ilivyokuwa mwaka 2006. Ongezeko la kasi ya ukuaji huo, lilitokana na kuimarika kwa uzalishaji viwandani, kufuatia upatikanaji wa umeme wa uhakika baada ya matatizo ya nishati hiyo mwaka 2006 kupungua na kuongezeka kwa uwekezaji katika maeneo maalum ya uzalishaji kwa kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, vipaumbele vya uzalishaji viwandani vitakuwa maeneo maalumu ya kuzalisha bidhaa za kuuza nchi za nje. Serikali pia italenga kutekeleza mikakati ya kuimarisha biashara na uwekezaji kwa ubia kati ya Tanzania na China, nchi nyingine za Asia na Mashariki ya Kati. Mkazo utaelekezwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini na kuhakikisha kwamba katika muda wa kati, hatutauza tena nje mazao ghafi, tukianza na pamba na korosho;

(ii) Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mauzo Nje;

(iii) Utekelezaji wa Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania 2020 *(Mini Tiger Plan 2020);*

(iv) Utekelezaji wa programu ya MKUMBITA[1]; na

(v) Kuweka mkazo katika mafunzo ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, shughuli za ujenzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 9.7 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 9.5 mwaka 2006. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na ongezeko katika shughuli za ujenzi wa barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; na uendelezaji wa ardhi. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.8 mwaka 2007, sawa na ilivyokuwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, mkazo katika shughuli za ujenzi ni kuwa na mtandao wa barabara zinazopitika katika kipindi chote cha mwaka, kwa kuhakikisha kuwa mikataba yote ya miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara inakamilishwa kwa wakati na katika ubora unaotakiwa.

Serikali itaweka mkazo pia katika kukarabati na kujenga barabara kuu za mikoa na barabara muhimu za vijijini. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha makazi katika miji na kupima na kuweka mipaka ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yatakayowekewa kipaumbele katika shughuli za kiuchumi za viwanda na ujenzi ni pamoja na:-

(i) Kuboresha upatikanaji na mtandao wa usambazaji maji mijini na vijijini;
(ii) Kukamilisha mchakato wa kuanzisha Hifadhi ya Mafuta ya Petroli;

(iii) Kuendeleza tafiti mbalimbali za upatikanaji wa nishati endelevu na ya uhakika; na

(iv) Kuweka utaratibu na kanuni mpya za uwekezaji katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utoaji huduma ni eneo la nne katika mgawanyo wa Pato la Taifa, ambazo zinajumuisha biashara na matengenezo, uchukuzi, mawasiliano, hoteli na migahawa, utawala, elimu, afya, huduma za fedha na bima na upangishaji majengo.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika huduma hizi kilikuwa asilimia 8.1 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2006. Mchango wa shughuli za huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 43.3 mwaka 2007, sawa na ilivyokuwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, shughuli za mawasiliano zilikua kwa kiwango cha asilimia 20.1 mwaka 2007, kulinganisha na asilimia 19.2 mwaka 2006. Sekta hii ndiyo iliyokua kwa kasi kubwa kuliko sekta nyingine zote za uchumi.

Hata hivyo, mchango wa sekta ya mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa mdogo sana (asilimia 2.3).

Mheshimiwa Spika, shughuli za huduma za uchukuzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.5 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2006. Ukuaji huu na biashara ya uchukuzi wa mizigo ya nchi jirani ambazo hazina bandari, reli na viwanja vya ndege na kuongezeka kwa safari za anga za ndani na nje ya nchi.

Mchango wa huduma za uchukuzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 4.2 mwaka 2007, karibu sawa na ule wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, kipaumbele katika shughuli za kiuchumi za mawasiliano na uchukuzi kitawekwa kwenye kuboresha mazingira ya kupanua ushiriki wa sekta binafsi katika uendeshaji na utoaji huduma za mawasiliano na uchukuzi.

Mheshimiwa Spika**,** kasi ya ukuaji katika shughuli za huduma ya elimu ilikuwa asilimia 5.5 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2006. Ukuaji katika shughuli za huduma za elimu ulitokana hasa na kuendelea kwa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Elimu za Msingi na Sekondari (*MMEM* na *MMES*); na kuongezeka kwa ajira mpya za Walimu.

Mheshimiwa Spika**,** Serikali itaendelea na mkakati wa kuboresha sekta ya elimu katika ngazi zote. Katika mpango wa muda wa kati, msukumo mkubwa wa Serikali kwa mwaka 2008/09 utaelekezwa katika kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Elimu za Msingi (*MMEM*) na Sekondari (*MMES*) hususan katika maeneo yafuatayo:-

(1) Kuongeza ujuzi na idadi ya Walimu na Wakufunzi, ili kuboresha uwiano wa Mwalimu na Wanafunzi katika ngazi zote, na kuongeza ubora wa elimu;

(2) Kujenga nyumba za Walimu, hususan kwenye maeneo yaliyo katika mazingira magumu na;

(3) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote, hasa nyenzo za kufundishia masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika**,** kiwango cha ukuaji katika huduma za afya kilikuwa asilimia 8.8 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2006. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na utekelezaji wa programu za chanjo, Malaria, Kifua Kikuu na *VVU/UKIMWI*.

Katika mwaka wa 2008/09, Serikali itaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya afya ya jamii na ya msingi, ukiwemo mkakati wa kutibu magonjwa ya watoto kwa uwiano na kuimarisha utafiti katika sekta ya afya. Serikali pia itatekeleza mkakati wa muda wa kati wa kupata vifaa vya kutibu magonjwa yote hapa nchini, na kuacha au kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nje kwa matibabu.

Mheshimiwa Spika**,** Kuhusu Maswala ya Mtambuka, makadirio ya idadi ya watu nchini kwa kutumia takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, yanaonyesha kuwa mwaka 2007 Tanzania ilikuwa na watu 39,446,061. Kati yao, wanaume walikuwa 19,352,480, au asilimia 49.0 na wanawake 20,093,581, au asilimia 51.0. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 38,291,219 Tanzania Zanzibar watu 1,154,842.

Mheshimiwa Spika, Idadi ya watu Tanzania inakua kwa asilimia 2.9 kwa mwaka, kiwango ambacho ni kikubwa na ni changamoto muhimu ya maendeleo. Kwa kutumia kasi hii ya ongezeko la watu inakadiriwa kwamba ifikapo mwaka 2025, Tanzania itakuwa na watu 63,516,735.

Mheshimiwa Spika**,** idadi ya watu nchini huleta changamoto katika kujenga uwezo wa kutoa huduma za jamii, hasa elimu, afya, maji, makazi na fursa za ajira. Katika mwaka 2008/09, Serikali itatoa elimu kuhusu Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu, ili kuhusisha masuala ya ongezeko la idadi ya watu na ukuaji wa Pato la Taifa; kutekeleza mkakati wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya Mwaka 2006; na kuendelea kusisitiza umuhimu wa kuzingatia vigezo (*variables*) vya masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo na bajeti.

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu nguvu kazi na ajira ni kwamba, kwa mujibu wa matokeo ya tafiti za awali za takwimu za ajira, imekadiriwa kwamba ajira mpya zipatazo 412,608 zilikuwa zimepatikana kwa kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Julai, 2005 hadi Disemba, 2007. Ajira 194,325 zimetokana na sekta rasmi, na ajira 218,283 zimetokana na sekta isiyo rasmi. Matokeo ya utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi ya mwaka 2007 yanatarajiwa kutoa idadi rasmi ya ajira mpya yatakapokamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu ijayo hadi mwaka 2010, malengo yafuatayo yamepangwa kutekelezwa:-

(1) Kuanza kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira na Mkakati wa Taifa wa Ajira;

(2) Kutekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ajira na;

(3) Kuendelea kuratibu mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kukuza ajira kila mkoa.

Mheshimiwa Spika**,** mwaka 2007, Serikali iliendesha Kampeni ya Kitaifa ya Upimaji wa Virusi Vya Ukimwi (*VVU*) kwa hiari katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kampeni hiyo ilikuwa na lengo la kuwafikia watu 4,170,659 ifikapo mwishoni mwa mwezi Novemba, 2007. Taarifa ya awali ya utekelezaji, inaonyesha kuwa jumla ya Watanzania waliojitokeza kupima *VVU* hadi tarehe 30 Aprili 2008 ni 4,211,727, sawa na asilimia 101 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, kati yao, wanaume walikuwa 1,863,188 sawa na asilimia 44.2 na wanawake 2,347,810 sawa na asilimia 55.8. Tathmini ya kampeni hiyo inaonyesha kuwa watu 194,149, sawa na asilimia takriban 4.6 ya watu wote waliopimwa, wakiwemo wanawake 117,254 na wanaume 76,895 wanaishi na *VVU* bila wao wenyewe kujitambua. Aidha, tathmini inaonyesha kuwa watu 38,041 sawa na asilimia 19.6 ya watu waishio na *VVU* wanahitaji tiba ya madawa ya kupunguza makali ya *VVU*.

Mheshimiwa Spika, utafiti kuhusu *UKIMWI* na magonjwa ya zinaa wa mwaka 2007, unaonyesha kuwa wastani wa kiwango cha maambukizi ni asilimia 7.4. Kiwango cha maambukizi kwa maeneo ya vijijini kilikuwa asilimia 6.0 kwa wastani, na Mijini asilimia 11.9. Katika kukabiliana na athari za janga hili, Serikali inaendelea na Mkakati wa Pili wa Kudhibiti Maambukizi ya *UKIMWI* kwa kipindi cha mwaka 2008 hadi 2012. Lengo kuu ni kuhimiza kinga, matunzo, na matibabu.

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu suala la Jinsia ni kwamba, katika mwaka 2007, Serikali ililenga kuendeleza mafunzo ya jinsia na kuingiza masuala ya jinsia katika sera, mipango na bajeti, sambamba na kuimarisha vitengo vya jinsia pamoja na kujenga mfumo wa kupima na kutathmini shughuli za wawakilishi wa masuala ya jinsia katika sehemu zao za kazi, Aidha, Serikali iliendeleza utoaji wa mikopo kwa wanawake na vijana na kuimarisha uhamasishaji wa masuala ya jinsia katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika kipindi cha 2008/09 ni pamoja na programu ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, kuimarisha vitengo vya jinsia katika ngazi zote na kuandaa Mkakati utakaoiwezesha nchi kufikia asilimia 50 ya uwakilishi wa wanawake katika ngazi zote za maamuzi na utendaji.

Mheshimiwa Spika**,** mwaka 2007, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Mazingira kwa kuandaa Kanuni, Miongozo na viwango vya usimamizi wa mazingira nchini pamoja na kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, kwa kufanya uperembaji wa utekelezaji wa Mkakati huo katika Mikoa ya Mbeya, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Lindi, Tabora, Kagera, Singida, Iringa, Manyara, Kigoma, Mwanza, Ruvuma na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Serikali katika kuhifadhi mazingira katika mwaka 2008/09 ni: kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mazingira na mikakati yake, na kukuza uelewa wa wananchi juu ya uhusiano kati ya mazingira, umaskini na maendeleo endelevu. Pia, Serikali inalenga kutekeleza mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa zinazohusu hifadhi ya mazingira, bila kuathiri mipango ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika**,** utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (*MKUKUTA*) umeonyesha mafanikio katika maeneo mengi ingawa kazi iliyobaki ni kubwa. Maeneo ya *MKUKUTA* ambayo yameonyesha matokeo mazuri ni pamoja na ukuaji wa Pato la Taifa, ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya ndani, usimamizi wa matumizi ya serikali, na utoaji wa huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza, Pato halisi la Taifa limekua kwa wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka katika kipindi cha miaka sita iliyopita. Hali hii inaashiria kuwa ukuaji halisi wa Pato la Taifa uko katika wigo uliokusudiwa, tukizingatia changamoto zinazotukabili. Ili tuwe na uchumi endelevu utakaopunguza umaskini wa kipato ni lazima tulenge kuukuza Uchumi kwa asilimia 8 na zaidi kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika**,** katika kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii, mafanikio makubwa yamepatikana katika utoaji wa huduma za jamii katika maeneo mbalimbali kama vile elimu, afya, upatikanaji wa maji na huduma za majitaka. Katika sekta ya elimu, kiwango halisi na cha jumla cha uandikishaji wanafunzi katika elimu ya msingi kiliendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali katika mwaka 2007/08, iliendesha kampeni ya kupanua elimu ya sekondari. Hatua hizi zimeongeza idadi ya wanafunzi wanaoingia sekondari kwa asilimia 84, kutoka wanafunzi 243,359 mwaka 2006 hadi 448,448 mwaka 2007**.** Elimu ya Juu pia imepanuka kwa kuwa na vyuo vikuu vingi vinavyoanzishwa, pamoja na shule za ufundi. Vile vile, kumekuwa na mafanikio makubwa katika huduma za maji safi na salama Vijijini na Mijini.

Mheshimiwa Spika**,** Katika mwaka 2007, Serikali iliendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya Mkakati wa Kupambana na Rushwa kwa kuanza kutekeleza rasmi Sheria mpya ya kuzuia na kudhibiti rushwa.

Aidha, mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Maadili kutoka kila Wizara na kila Halmashauri yalitolewa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imerekebisha kifungu cha sheria kinachoelekeza utoaji wa hukumu katika muda usiozidi siku 90 baada ya kesi kusikilizwa. Idadi ya Mawaziri na Wabunge wanawake imeendelea kukua na katika mwaka 2008/2009, Serikali inalenga kuboresha uwezo wa utendaji wa vyombo vya kulinda sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini, na kuleta ustawi wa jamii kwa kutumia programu mbalimbali za maendeleo ya kisekta na Mikoa zitakazozingatia maeneo makuu matatu ya *MKUKUTA*. Maeneo hayo makuu ni ukuaji uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, uimarishaji wa hali ya maisha na maendeleo ya jamii, na utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania 2020(*Tanzania Mini-Tiger Plan 2020*) ni kwamba katika mwaka 2007, ujenzi wa Kanda Maalum ya Uwekezaji ya Benjamin William Mkapa iliyopo Mabibo, Dar es Salaam uliendelea kwa kukamilisha miundombinu ya barabara, maji na umeme.

Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Kanda Maalum ya Uwekezaji wa Habari na Teknolojia ya Mawasiliano (*ICT-SEZ*) ulikamilika na maandalizi ya ujenzi wa Kanda

hiyo yanaendelea. Vile vile, Serikali itaendelea kutekeleza mipango yake ya kuanzisha maeneo maalumu ya uwekezaji katika mikoa ya Tanga, Kigoma na Pwani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007, Serikali iliendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF* II). Lengo la awamu hii ya pili ni kuiwezesha jamii kupata fursa ya kusimamia utekelezaji wa miradi midogo inayoibuliwa na jamii husika, na ambayo itachangia katika kuboresha hali ya maisha ya wananchi kulingana na malengo yaliyoainishwa katika viashiria vya malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya *CCM*, Milenia na *MKUKUTA*.

Mheshimiwa Spika**,** awamu ya pili inatekelezwa katika Halmashauri zote za Tanzania Bara, na mbili Tanzania Zanzibar. Awamu hii inashughulikia mikakati miwili; Mfuko wa Taifa wa Vijiji na Mkakati wa Kujenga Uwezo. Walengwa wakuu katika Mfuko wa Taifa wa Vijiji ni jamii zinazokosa huduma za kijamii na kimasoko; jamii zisizo na uhakika wa chakula; na jamii zinazoishi katika mazingira hatarishi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kujenga Uwezo, walengwa wakuu ni mawakala wanaosaidia jamii katika kutumia rasilimali za Mfuko wa Taifa wa Vijiji na watu binafsi walio maskini wanaojihusisha na vikundi vya akiba.

Mheshimiwa Spika**,** mwaka 2007, Serikali iliendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ambapo Tanzania ilipanda daraja na kushika nafasi ya 130 kati ya nchi 178 duniani katika kupunguza gharama za kufanya biashara ikilinganishwa na nafasi ya 142 kati ya nchi 175 mwaka 2006. Aidha, gharama za kufanya biashara nchini zilipungua kutoka asilimia 161.3 mwaka 2006 hadi asilimia 91.7 mwaka 2007. Kitengo cha Kanuni Bora za Biashara *(Better Regulation Unit*) kilifanyiwa marekebisho katika utendaji wake wa kazi kwa kuongezewa majukumu mapya ili kiweze kurahisisha utoaji wa huduma kwa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika**,** Serikali iliendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa sekta binafsi kwa kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (*MKUMBITA*) kwa lengo la kupunguza gharama za uanzishaji na uendeshaji wa biashara kwa kuondoa vikwazo vikiwemo vya kisera, kisheria, kanuni, kiutaratibu na kitaasisi ambavyo vinakwamisha ukuaji wa sekta binafsi. Katika mwaka 2007, mafanikio kadhaa yamejidhihirisha katika maeneo mawili:-

(1) Serikali ilianza rasmi kutekeleza Mradi wa Kuongeza Ushindani katika Sekta Binafsi. Mradi huu unalenga kuongeza ushindani, hususan baina ya wajasiriamali wadogo kabisa, wadogo na wa kati, kwa kupunguza gharama za kufanya biashara, kujenga uwezo miongoni mwa makampuni ya ndani ili kuyawezesha kuhimili ushindani katika soko la kimataifa.

(2) Mchango wa sekta binafsi katika ukuzaji rasilimali ulikuwa asilimia 72.1 ukilinganisha na asilimia 69.9 mwaka 2006. Serikali itaendelea kutekeleza

Mkakati wa Maendeleo ya Sekta Binafsi, kama sehemu ya juhudi zake za kukuza maendeleo ya sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika**,** mwaka 2007, Baraza la Taifa la Biashara lilifanya mikutano miwili (*Investors' Round Table*) kwa wawekezaji wa ndani na nje. Aidha, katika kipindi hicho Baraza liliandaa warsha tatu kwa ajili ya Kamati Kuu na Sekretariati katika Ukanda wa Magharibi (Tabora na Kigoma); Ukanda wa Kati (Morogoro, Dodoma na Singida) na Ukanda wa Kusini (Mtwara na Lindi). Baada ya kukamilisha zoezi la kuanzisha Mabaraza ya Biashara katika ngazi ya Mkoa, jitihada sasa zinaelekezwa katika uanzishwaji wa Mabaraza ya Biashara katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia *MKURABITA* inalenga kuhakikisha kuwa biashara na rasilimali za wananchi zilizo kwenye sekta isiyo rasmi zinarasimishwa ili ziweze kutambulika kisheria na hivyo kuwawezesha wamiliki kuzitumia rasilimali hizo kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo. Katika mwaka 2008/2009, maeneo ambayo yataendelea kufanyiwa kazi chini ya programu hii ni kama ifuatavyo:-

(1) Kuandaa utaratibu wa kasi zaidi *(fast tracking)* wa kurasimisha ardhi za vijiji na kutoa hati miliki;

(2) Kuandaa utaratibu wa kasi zaidi wa kurasimisha ardhi za mijini kwa baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara;

(3) Kupanua wigo wa majaribio ya matumizi ya rasilimali katika kupata mikopo *(mortgage finance)* katika jiji la Arusha, Mbeya, na Zanzibar;

(4) Kutafiti mifumo mipya ya usajili wa biashara ili kuimarisha utawala bora katika shughuli za biashara na;

(5) Kusimamia uanzishaji na utekelezaji wa Mfuko Maalum kwa ajili ya shughuli za kurasimisha raslimali nchini.

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2007, Awamu ya Pili ya Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira ilizinduliwa rasmi. Kupitia programu hii, taasisi za fedha 13 ziliidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania kutoa mikopo kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 3 Machi, 2008, taasisi 9 zilikuwa tayari zimepewa mikopo kupitia programu hii. Katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya programu hii, Serikali iliupatia Mfuko wa Dhamana shilingi billioni 10.5 kwa ajili ya Benki za *CRDB* na *NMB*. Benki hizo zilikubali kutoa mikopo mara tatu ya kiasi kilichotolewa na Serikali, na zilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 32.3.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwahamasisha wananchi kujiunga katika vyama vya kuweka na kukopa *(SACCOS)* ili kuongeza fursa za kupata mikopo

katika taasisi za fedha na programu za Serikali. Kati ya Julai 2006 na Aprili 2008, idadi ya Vyama vya Ushirika wa Kuwepo na Kukopa imeongezeka kwa asilimia 120, kutoka vyama 2,028 hadi 4,445. Vyama hivyo vimekusanya akiba ya shilingi bilioni 74.6, na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 186.6.

Mheshimiwa Spika**,** misingi na malengo ya uchumi na maendeleo ya jamii katika kipindi cha muda wa kati (2008/2009 - 2010/2011)ni kwamba, baada ya maelezo ya mapitio ya hali ya uchumi kwa mwaka 2007, naomba nieleze misingi ya malengo *(assumptions)* ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kwa kipindi cha muda wa kati (2008/2009 – 2010/2011) Misingi hiyo ni pamoja na hii ifuatayo:-

(1) Kuendelea kutengemaza vigezo muhimu vya uchumi jumla, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa Pato la Taifa, kuthibiti mfumuko wa bei, kukusanya mapato ya ndani, na viwango vya ubadilishaji wa fedha;

(2) Kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa MKUKUTA, kwa kuelekeza rasilimali zaidi katika maeneo yatakayokuza uchumi kwa haraka katika kipindi cha muda wa kati;

(3) Ukuaji wa shughuli za kiuchumi za kilimo (mazao, mifugo, uwindaji na misitu) unategemea kuongezeka kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu vijijini na upatikanaji wa mikopo vijijini kupitia vyama vya kuweka na kukopa *(SACCOS)*, mifuko mbalimbali ya kutoa mikopo, na mikakati mingine ya kisera;

(4) Kuendelea kuboresha na kuimarisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii, na kulinda mafanikio ya jumla yaliyokwishapatikana;

(5) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutokana na maboresho ya mfumo na usimamizi wa kodi, na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji na biashara rasmi;

(6) Mapato ya nje, ikiwemo misaada na mikopo yenye masharti nafuu inatarajiwa kuendelea kupatikana;

(7) Kuendelea kuboresha mazingira ya ukuaji wa sekta binafsi;

(8) Kuimarisha sera za ujazi wa fedha ambazo zitajionyesha katika kiwango cha chini cha mfumuko wa bei, kushusha riba ya mikopo ya benki, na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; na

(9) Kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika harakati za kukuza uchumi na maendeleo ya jamii kupitia serikali zao za mitaa.

Mheshimiwa Spika, malengo ya uchumi jumla katika mwaka 2008/2009 - 2010/2011, yatakuwa yafuatayo:-

(1) Pato la Taifa halisi litakua kwa asilimia 7.8 mwaka 2008, asilimia 8.1 mwaka 2009, na asilimia 8.8 mwaka 2010 na kuongezeka hadi asilimia 9.2 mwaka 2011;

(2) Mfumuko wa bei utadhibitiwa ili uwe chini ya asilimia 7.0, ifikapo mwishoni mwa Juni 2009;

(3) Mapato ya ndani yafikie asilimia 18.5 ya pato la Taifa mwaka 2008/09, asilimia 18.6 mwaka 2009/10 na asilimia 19.0 mwaka 2010/2011;

(4) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana, ( (M) katika wigo wa asilimia 23.9 mwaka 2008/2009 na asilimia 22.9 mwaka 2009/2010, kulingana na malengo ya ukuaji wa uchumi, na kasi ya upandaji bei;

(5) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kulipia mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano;

(6) Kuwa na kiwango cha kubadilisha fedha kitakachofuata mwenendo wa soko la fedha (IFEM); na

(7) Kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo katika sekta ya fedha ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea hali ya uchumi wa Taifa, matarajio, misingi na malengo ya mpango katika kipindi cha mwaka 2008/2009 hadi 2010/2011 ni wazi kwamba hatua zilizochukuliwa na Serikali kwa kiasi kikubwa zimeweza kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Juhudi kubwa zinaendelea kuelekezwa katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi unamnufaisha mwananchi wa kawaida kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha hilo hatuna budi kutambua kuwa tunakabiliwa na changamoto nyingi. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(1) Hivi sasa uchumi wetu upo katika hali ngumu kutokana na kupanda kwa kasi kwa bei ya mafuta ya petroli, mbolea na malighafi za viwandani. Tunalazimika kuchukua hatua za dhati kuzalisha chakula cha kutosha ili kujihami na madhara ya changamoto hiyo;

(2) Kwa kuzingatia kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa asilimia 2.9 kwa mwaka, inatulazimu kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ili pato la kila mwananchi liongezeke;

(3) Miundombinu hasa barabara, reli, bandari na umeme bado haitoshelezi mahitaji ya kutuwezesha kutumia fursa ya nchi yetu kuwa kiungo muhimu kibiashara na nchi zinazotuzunguka ambazo hazina bandari;

(4) Hatua za kuwezesha wajasiriamali zimeanza kuleta matunda. Hata hivyo, uwezo wa Serikali kuendelea na mpango huu kwa kiwango kikubwa ni mdogo. Kuna haja ya kupanua uwezo kwa kuviimarisha na kuvihamisha zaidi vyombo vya fedha ili kuchukua dhima hii hasa ikizingatiwa kuwa matokeo ya awamu ya kwanza na ya pili yanatia moyo kutokana na marejesho mazuri ya mikopo iliyotolewa;

(5) Bajeti ya Serikali inaendelea kuwa tegemezi kwa misaada ya nje kwa kiasi kikubwa. Pamoja na nia njema inayoonyeshwa na wahisani kuendelea kutusaidia ni lazima tuongeze mapato ya ndani sanjari na kudhibiti matumizi ya kawaida kwa fedha zetu wenyewe kwa kuanzia na baadaye sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo pia ilipiwe na fedha zetu wenyewe;

(6) Mahitaji ya fedha za kigeni katika uchumi bado ni makubwa kuliko uwezo wetu wa kuuza bidhaa na huduma nje. Ni muhimu sana kuweka msukumo zaidi katika kukuza mauzo nje ya bidhaa na huduma kama mbinu muhimu ya kujenga uwezo wetu wa kujitegemea;

(7) Taratibu za kuanzisha na kuendesha uwekezaji na biashara bado una gharama kubwa na hivyo kudhoofisha juhudi za kufanikisha azma hii. Ni muhimu tujidhatiti katika kuboresha mazingira ya biashara;

(8) Mpango wa Kuharakisha Maendeleo Tanzania *(Tanzania Mini-Tiger Plan)* unaendelea kwa kasi ndogo. Tunalazimika kurekebisha hali hii ili tupige hatua zaidi;

(9) Uwezo *(Capacity)* wa watumishi kufanikisha majukumu na malengo ya Serikali unahitaji kuimarishwa kwa kuongeza idadi ya watumishi katika Sekta za kipaumbele – hasa elimu na afya, na kuwapatia mafunzo muhimu ili kuwapa ujuzi unaotakiwa;

(10) Kutokana na hali mbaya ya chakula duniani inayosababisha kupanda kwa bei, ni muhimu kuhakikisha tunazalisha zaidi na kuhifadhi chakula cha kutosha pamoja na kutumia tatizo hili kama fursa ya kuzalisha mazao ya chakula kwa kiwango kikubwa na kuuza nje ziada;

(11) Riba za mikopo ya benki bado ni kubwa na hivyo kuathiri uwezo hasa wa wajasiriamali kukopa na kufanya biashara yenye tija, na kuwanufaisha walengwa. Mafanikio yaliyoanza kuonekana katika kushusha riba hayanabudi kuendelezwa;

(12) Kutokana na umuhimu wa kilimo katika kubeba maslahi ya zaidi ya asilimia 80 ya wananchi, kuna haja ya kukusanya nguvu za Serikali na sekta binafsi

kwa pamoja ili kuongeza tija katika sekta hii. Serikali itaendelea kuzingatia changamoto hizi katika mipango yake ya kila mwaka, kadiri uwezo wake utakavyoendelea kuimarika. Aidha, ni muhimu kwa kila mwananchi na taasisi kutoa mchango wake katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto nilizozieleza.

Mheshimiwa Spika**,** kwa kumalizia naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliotusaidia, Nchi marafiki na Masharika ya Fedha ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Ninapenda nizitaje baadhi ya nchi na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa kama ifuatavyo:-

Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*); Benki ya Maendeleo ya Afrika; Mashirika mbali mbali ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNDP, UNESCO, UNFPA, UNHCR, UNICEF, UNIFEM, FAO, IFAD, WFP* na *WHO, ILO* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Kamisheni ya Nchi za Ulaya, Mfuko wa *OPEC* (*OPEC Fund*), *BADEA*, Abu Dhabi *Fund*, Serikali za Norway, Marekani, Sweden, Finland, Canada, Denmark, Japan, Uswisi, Uholanzi, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Hispania, China, Korea, Kuwait, Italia, Ireland, na nchi nyingine marafiki na mashirika mbalimbali ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*).

Mheshimiwa Spika**,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Waheshimiwa Wabunge kama ilivyo kawaida kwa situ kama hii hatuanzi na kupokea taarifa za Kamati na taarifa ya Kambi ya Upinzani na kadhalika.

Kwa sababu hotuba hii ni kama utangulizi wa hotuba ya saa kumi, kwa hiyo, natangaza kwamba hadi sasa nimeshapata orodha ya wachangiaji 43, kutakuwa na fursa ya kuzungumza kwa sababu tutaanza Jumatatu na tutaendelea hadi Ijumaa.

Wakati natangaza waliopo nimepata taarifa kuwa yupo Dr. Enos Bukuku Naibu Gavana wa Benki Kuu wa kwanza, karibú sana Dr. Bukuku.

Baada ya hayo sasa Waheshimiwa Wabunge, naomba kutangaza kuwa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili na siyo saa kumi na moja.

*(Saa 05.30 Asubuhi Bunge lilisimamishwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waziri wa Fedha, kwa ajili ya hoja ya Makadirio na Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. Waheshimiwa Wabunge, huu ni utaratibu mpya tumeuona ni mzuri zaidi kuliko kumkuta Waziri wa Fedha humu ndani. Kuanzia sasa atakuwa akisindikizwa baada ya kuitwa akitokea nje. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009**

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, vipo vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu za bajeti. Kitabu cha kwanza, kinahusu makisio ya mapato, kitabu cha pili na cha tatu ni vya makisio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri za Miji na Wilaya, kitabu cha nne kinaelezea Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa, pamoja na Halmashauri. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2008, ambao ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya bajeti yamehusisha taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali na wadau wengine. Kama ilivyokuwa mwaka jana, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walipata fursa ya kujadili Mwongozo wa Mpango na Bajeti mapema mwaka huu na kutoa maoni yao hasa kuhusu vipaumbele vya bajeti hii ya mwaka 2008/2009.

Mwongozo wa Serikali wa Mpango na Bajeti ni hatua muhimu katika maandalizi ya bajeti, kwa kuwa unatoa fursa kwa wadau na hasa Waheshimiwa Wabunge kutoa michango yao mapema kabla mapendekezo ya bajeti hayajakamilika na kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa rasmi. Kwa niaba ya Serikali, nachukua nafasi hii kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge kwa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa katika bajeti hii. Utaratibu huu utakuwa wa kudumu, na tutautumia kwa pamoja kuweka mikakati itakayoharakisha utekelezaji wa ahadi ya Chama Tawala ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya bajeti hii. Napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda - Mbunge wa Handeni, kwa kazi nzuri ya kuchambua mapendekezo ya bajeti kwa undani na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali ya bajeti hii. Ushauri wa Kamati hii umesaidia sana katika kuboresha bajeti ninayoiwasilisha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Wizara zote, Idara zinazojitegemea, Mikoa, Serikali za Mitaa, taasisi za kitaifa na kimataifa na wawakilishi

wa sekta binafsi kwa michango yao iliyosaidia kufanikisha maandalizi ya bajeti hii. Naishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2008 na nyaraka mbalimbali za kisheria ambazo ni sehemu ya bajeti hii.

Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Uchumi, nikianza na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Jeremia S. Sumari (Mb) na Mheshimiwa Omari Y. Mzee (Mb.); Katibu Mkuu, Gray S. Mgonja, Naibu Makatibu Wakuu; Ramadhani M. Khijjah, John M. Haule na Laston T. Msongole, Wakuu wa Idara, Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati.

Mwisho nawashukuru kipekee wataalamu na wale wote waliotoa mapendekezo kuhusu sera, mikakati na masuala mbalimbali ya kodi ambayo yamezingatiwa kwa kiasi kikubwa katika bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Fedha kabla yangu Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji (Mb) na aliyekuwa Naibu wake Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib (Mb). Napenda pia kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji - Mheshimiwa Juma Alifa Ngasongwa (Mb) na aliyekuwa Naibu wake Mheshimiwa Gaudence Kayombo (Mb) kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuongoza. Zilizokuwa Wizara mbili. *(Makofi)*

Nimejifunza mengi kutoka kwao ambayo yananisaidia katika kuongoza Wizara hii mpya ya Fedha na Uchumi. Nawatakia afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilitoa maelezo ya mapitio ya utekelezaji wa sera za uchumi jumla katika mwaka wa 2007/2008 na mtazamo wa Serikali kuhusu hali ya uchumi katika muda wa kati (2008/2009 – 2010/2011).

Sasa napenda nitoe maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Sera za Bajeti ya mwaka 2007/2008 hasa katika kipindi cha miezi tisa ya kwanza ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, bajeti ya mwaka 2007/2008 imetekelezwa kwa msingi wa sera mbalimbali zilizotangazwa wakati wa kuwasilisha bajeti hiyo Bungeni mwezi Juni 2007. Sera hizo ni pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, kuimarisha mgawanyo wa fedha za bajeti kwa mujibu wa vipaumbele vya Ilani ya Uchaguzi wa CCM na MKUKUTA, usimamizi mzuri wa matumizi ya Serikali na uwajibikaji. Maelezo kamili ya utekelezaji wa sera hizo yanafuata.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa miezi tisa ya kwanza ya mwaka wa 2007/2008 ni pamoja na haya yafuatayo:

(i) Bajeti yetu iliendelea kuwa tegemezi kwa misaada ya nje kwa kiasi kikubwa licha ya mapato ya ndani kuendelea kukua. Kwa hiyo, changamoto ya kwanza

mwaka 2008/2009 ni kuongeza mapato ya ndani na kudhibiti kukua kwa haraka kwa bajeti ya kawaida ili tuanze kujitegemea.

(ii) Mchango wa mapato yasiyo ya kodi katika bajeti ni mdogo tukizingatia fursa zilizoko za kukusanya mapato mengi kutoka kwenye maeneo hayo. Serikali inaandaa mkakati maalumu wa kuimarisha vyanzo hivyo vya mapato.

(iii) Hata hivyo, mapato ya kodi yanakusanywa kama yalivyolengwa na matarajio ni kwamba tutafikia malengo ya makusanyo ya mwaka mzima wa 2007/2008 bila ya wasiwasi wowote.

(iv) Taratibu za ununuzi wa Umma bado zinasumbua taasisi nyingi katika utekelezaji wa bajeti. Mpango wa kuviimarisha vitengo vya ununuzi Serikalini unaandaliwa. Aidha, mpango mkakati wa kujenga taaluma ya ununuzi wa umma unaandaliwa.

(v) Kwa ujumla wake, matumizi ya Serikali yanaendelea kulingana na bajeti na inatarajiwa kwamba bajeti ya 2007/2008 itakuwa imetekelezwa kama ilivyoidhinishwa na Bunge, isipokuwa maeneo kadhaa yaliyofanyiwa uhamisho wa ndani kukidhi mahitaji ya dharura.

Mheshimiwa Spika, yako pia maeneo mengine ambayo Serikali iliahidi kuyatekeleza katika mwaka huu wa fedha unaokaribia kwisha. Ningependa kutoa maelezo mafupi ya utekelezaji wa ahadi hizo za Serikali kama ifuatavyo:

(vi) Serikali ilitangaza kwamba ilikusudia kuondoa fedha zake zinazowekwa katika benki za biashara na kuzihamishia Benki Kuu ili benki zisitumie fedha za Serikali kununulia dhamana za muda mfupi za Serikali *(Treasury Bills)*, utaratibu ambao Serikali ilijikuta inalipa riba kwa fedha zake yenyewe. Sehemu kubwa ya fedha za Serikali katika amana zilizoko kwenye benki za biashara ni fedha za misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Hatua ambazo zimeshachukuliwa katika zoezi hilo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(a) Serikali imeshatambua na kuhakiki akaunti zinazohusika.

(b) Serikali imeanza majadiliano na wahisani wanaochangia katika tatizo hili.

(c) Tumetambua mahitaji ya Benki Kuu ili iweze kuhimili usimamizi wa akaunti hizo zitakazofunguliwa hapo na kuhakikisha kuwa Benki hiyo itaweza kutoa fedha hizo kwa wakati zitakapohitajika kwenda kwenye miradi.

(d) Utaratibu wa kufungua akaunti mpya Benki Kuu za miradi ya Serikali umeanza.

(i) Serikali imeanza kutumia mfumo wa kisasa wa malipo *Tanzania Interbank Settlement System (TISS)* kwa majaribio, ili hatimaye mfumo huo utumike na kuondoa umuhimu wa akaunti za Serikali kuwa na fedha nyingi katika benki za biashara.

Mfumo huu tayari unatumiwa na Mamlaka ya Mapato, katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka kwa walipakodi wakubwa. Aidha, Serikali inajiandaa kutumia mfumo huu wakati wa utekelezaji wa miradi itakayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la *Millenium Challenge Corporation (MCC).*

Miradi hiyo itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha ujao (2008/2009). Chini ya mfumo huo, fedha za malipo ya ujenzi wa miradi husika zitaingizwa na kutumwa moja kwa moja kwenye akaunti bila kuandika hundi za malipo. Mfumo huu wa malipo unapunguza matumizi ya hundi na ya fedha taslimu.

(ii) Katika juhudi za kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, Serikali, kupitia *TRA*, imefanya uchambuzi wa misamaha ya kodi kwa lengo la kuipunguza ili kuokoa mapato ya Serikali. Uchambuzi huo umebaini kwamba misamaha yote ya kodi inatolewa kwa mujibu wa Sheria. Sehemu kubwa ya misamaha inatolewa kwa wawekezaji katika sekta ya madini chini ya Sheria ya Madini na Mikataba husika, wawekezaji katika sekta nyingine wanaopewa Hati za Vivutio kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* chini ya Sheria ya Uwekezaji.

Kundi lingine linalofaidika na misamaha ya kodi ni lile la Mashirika ya dini na asasi zisizo za Serikali na hasa zile zinazotoa huduma kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Hata hivyo, kodi zinazosamehewa kwa kundi hili zinalipiwa na Serikali kwa utaratibu wa Hati ya Hazina *(Treasury Voucher System). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa inatafakari na kuainisha marekebisho ya Sheria mbalimbali ambayo yatahitajika yafanywe ili kupunguza misamaha ya kodi na kuokoa mapato ya Serikali. Zoezi hili linaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato inaendelea kutoa elimu ya biashara na kodi kwa walipa kodi wadogo ili kuwawezesha wapate ufahamu wa kutosha kuhusu biashara na ukokotoaji wa kodi. Mamlaka imekua ikitoa machapisho mengi yenye maelezo kuhusu maadili ya biashara, ujasiriamali na ulipaji wa kodi – hasa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* na kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua ambazo Serikali inachukua – kwa mfano kupunguza matumizi ya hatifungani za Serikali katika soko la fedha na dhamana za Serikali, uamuzi wa Serikali wa kupunguza kiasi cha fedha zake kinachokaa katika benki za biashara na usimamizi mzuri wa Soko la Dhamana za Serikali, riba za mikopo ya benki zimeanza kushuka na inategemewa kwamba zitaendelea kushuka.

Aidha, Sheria ya Ukopeshaji Vifaa *(Finance Leasing)* imetungwa ili kuweka mazingira yatakayowezesha wananchi kupata mitambo na vifaa vya uzalishaji, usafirishaji, ujenzi, nakadhalika kwa njia ya kukodi. Aidha, zoezi la kuainisha marekebisho yanayotakiwa katika Sheria mbalimbali ili kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha vyombo vya fedha vitoe mikopo ya nyumba, limekamilika.

Mapendekezo ya marekebisho mbalimbali ya Sheria husika yataletwa Bungeni katika mwaka ujao wa 2008/09. Pamoja na hatua hizi, viko vyombo vya fedha ambavyo vinatoa mikopo ya nyumba kwa kutumia sheria zilizoko hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilidhamiria kwamba katika kipindi cha miaka mitatu, itaongeza mtaji katika Benki ya Rasilimali *(TIB)* ufikie angalau shilingi bilioni 50. Dhamira hiyo Waheshimiwa Wabunge, sasa imekamilika. Bajeti ya 2008/2009 imetenga shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuimarisha mtaji wa TIB, ambao utafika shilingi bilioni 50. Uamuzi huu wa Serikali ni wa makusudi kwa kutambua tatizo kubwa la ukosefu wa mikopo ya uzalishaji katika viwanda na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuimarisha mtaji wa benki hii, Serikali itaelekeza nguvu katika Benki ya Posta ambayo pia ni Benki ya Umma. Zoezi la kuirekebisha benki hiyo linaendelea. Tathmini ya awali ya Benki ya Posta ilionyesha kwamba benki hiyo ilihitaji iimarishwe kimfumo na kiutendaji, kwanza ndipo ifanyiwe uamuzi kuhusu majukumu yake katika uchumi wa nchi.

Kazi ya benki hiyo kujiimarisha inaendelea ambayo ni pamoja na kuongeza matumizi ya teknolojia, kufungua matawi mapya, kuongeza wateja na amana na kubuni huduma mpya *(new products)*. Hivi sasa Benki ya Posta inajiendesha vizuri na mkakati wa kuimarisha benki hiyo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuuza kwa wananchi asilimia 21 ya hisa za Serikali katika Benki ya *NMB* linakaribia kukamilika, baada ya hesabu za mwaka 2007 kukaguliwa. Kwa kuwa zoezi hili litakamilika baada ya Juni, 2008, mapato yatokanayo na uuzaji wa hisa hizo yataingia katika bajeti ya Serikali ya 2008/2009. Mapato hayo yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 60 baada ya kuondoa gharama zinazokadiriwa kufikia shilingi bilioni 5.

Aidha mchakato wa kurekebisha na kubinafsisha Shirika la Bima la Taifa, unaendelea kwa utaratibu wa kutenganisha majengo na biashara ya bima, badala ya utaratibu wa mwanzo ambao ulikuwa unachanganya biashara ya bima na majengo ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeainisha utaratibu wa kuzitaka Wakala, Taasisi na Mashirika ya umma kuchangia katika bajeti ya Serikali kwa utaratibu utakaokubalika, kama nitakavyoeleza baadaye. Aidha, utaratibu wa Retention wa Wizara na Idara zinazokusanya maduhuli ya Serikali na kubakiza kiasi fulani cha mapato, umeimarishwa na sasa utatoa fursa nzuri kuwawezesha wale wanaokusanya maduhuli makubwa wasirudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Ndani katika bajeti ya mwaka 2007/2008, Serikali ilikusudia kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kurekebisha mfumo wa kodi na taratibu za kusimamia ukusanyaji mapato ili kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi bilioni 3,502.583 (trilioni 3.5), sawa na asilimia 18.1 ya Pato la Taifa kwa takwimu zilizokuweko wakati huo, ikilinganishwa na asilimia 14.3 mwaka 2006/2007. Kufuatia

mabadiliko ya takwimu za Pato la Taifa, kiwango hicho cha asilimia 18.1 sasa ni sawa na asilimia 16.7.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizochukuliwa ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ni pamoja na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kupanua wigo wa kodi, na kusajili walipa kodi wapya.

Aidha, chini ya Mpango Mkakati wa Pili wa Mamlaka ya Mapato *(TRA Second Corporate Plan)* kumekuwa na maboresho katika usimamizi, utendaji na uwajibikaji wa *TRA*.

Kama nilivyosema awali, Serikali imeanza kutathmini mchango wa mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara na Idara mbalimbali zinazokusanya mapato hayo, ili kubaini mapungufu na kufanya marekebisho yanayofaa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*, Sura 148. Marekebisho haya yalitoa unafuu wa kodi kwa pamba za usafi wa watoto *(pampers)*, na mitungi ya kuzimia moto kwa nia ya kuhamasisha matumizi yake. Aidha, Serikali ilipunguza kiwango cha chini cha kukokotoa kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 18.5 hadi asilimia 15, ili kupunguza mzigo wa kodi kwenye kipato cha wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda thamani halisi ya mapato, Serikali pia ilirekebisha viwango vya ushuru wa Bidhaa sanjari na kasi ya kupanda kwa fahirisi ya bei.

Vile vile, Serikali iliongeza ushuru wa mafuta ya petroli na kurekebisha mfumo wa kutoza ada ya mwaka ya leseni za magari ili kuongeza uwezo wa Mfuko wa Barabara kumudu ongezeko la gharama za matengenezo ya barabara. Kwa ujumla matokeo ya hatua hizo yameonyesha mafanikio kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani kwa kipindi cha Julia, 2007 hadi Machi, 2008 yalifikia shilingi bilioni 2,656.2, ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 2,633.9 katika kipindi hicho, sawa na asilimia 100.8 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, kodi ya mapato ya ajira *(PAYE)* na kodi ya mapato ya makampuni na pia tozo ya kuendeleza ufundi stadi *(Skills Development Levy)* zimekuwa na mchango mkubwa katika mwenendo huu mzuri wa makusanyo ya mapato. Kwa upande mwingine, ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara na Idara mbalimbali za Serikali, pamoja na ushuru na kodi zinazokusanywa kutoka bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, sio wa kuridhisha.

Hata hivyo, pamoja na vianzio hivyo vya mapato kutokufikia malengo, Mamlaka ya Mapato ilivunja rekodi yake kwa kukusanya shilingi bilioni 328.6 katika mwezi wa Desemba, 2007. Kiwango cha juu kilichowahi kukusanywa na *TRA* kabla ya Desemba, 2007 kilikuwa shilingi bilioni 259 zilizokusanywa mwezi Machi 2007.

Mwenendo huu mzuri ni matokeo ya usimamizi thabiti wa utawala wa kodi katika *TRA*, utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Pili wa Mamlaka ya Mapato na hatua mbalimbali za mapato ambazo zilipitishwa na Bunge katika bajeti ya mwaka huu wa 2007/2008. Aidha, Mpango Mkakati wa Tatu wa *TRA* utaweka mkazo, pamoja na mambo mengine, katika kuongeza ukusanyaji wa ushuru na kodi za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nje katika kipindi cha Julai, 2007 hadi Machi 2008 ilifikia shilingi bilioni 1,873.781, ambayo ni asilimia 80 ya makadirio ya mwaka mzima. Fedha hizo ni pamoja na misaada na mikopo ya bajeti *(General Budget Support – GBS)* ambayo ilikuwa shilingi bilioni 956.038, zilizokwishatolewa na ambazo ni asilimia 8 zaidi ya makadirio ya mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, hali hii imetokana na sababu kuu mbili: ya kwanza ni kwamba fedha za Benki ya Maendeleo ya Afrika zilizotegemewa kuingia mwaka 2006/2007, zilichelewa kutolewa na, zikaingia katika Akaunti ya Serikali mwaka huu wa fedha.

Pili, Wahisani wengi walitoa sehemu kubwa ya misaada yao ya bajeti mwanzoni mwa mwaka wa fedha sanjari na makubaliano chini ya Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania *(MPAMITA).*

Aidha, misaada na mikopo ya kisekta na programu maalum *(basket funds)* kwa kipindi cha Julai, 2007 hadi Machi 2008 ilikuwa shilingi bilioni 383.786 ambazo ni asilimia 33 zaidi ya makisio ya mwaka mzima. Kwa upande mwingine, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilifikia shilingi bilioni 533.957 katika kipindi cha Julai, 2007 hadi Machi 2008, sawa na asilimia 60 ya makisio katika kipindi hicho. Hii imetokana na kasi ndogo ya utekelezaji wa baadhi ya miradi kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, matumizi, katika kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ya mwaka wa fedha 2007/2008, mwenendo wa bajeti kwa ujumla ni wa kuridhisha. Matumizi ya jumla yanaendelea kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, utekelezaji wa bajeti umekabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwemo mfumuko wa bei unaotokana na kupanda kwa bei ya chakula, bei ya mafuta ya petroli, na bei ya mbolea katika soko la dunia.

Serikali imechukua hatua kadhaa kukabiliana na changamoto hizi. Hatua hizo ni pamoja na kufuta ushuru wa mahindi kutoka nje ya nchi ili kutoa motisha kwa wafanyabiashara kuagiza mahindi kutoka nje. Hata hivyo hatua hii haikufanikiwa kwa kuwa nafaka hazipatikani katika masoko duniani kote.

Aidha, kutokana na upungufu mkubwa wa saruji, Serikali ilipunguza ushuru wa saruji ili kuhamasisha uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje kuziba pengo. Hatua zaidi za kukabiliana na tatizo la ukosefu wa chakula zitaelezewa na Waziri wa Sekta hiyo, atakapowasilisha sera na bajeti ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa Machi, 2008, jumla ya matumizi ya Serikali ilikuwa shilingi bilioni 4,147.415 (trilioni 4.147) ikilinganishwa na makisio ya shilingi bilioni 4,836.919 (trilioni 4.836) katika kipindi hicho. Shilingi bilioni 2,451.925 (trilioni 2.452) ni matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 1,695.491 (trilioni 1.695) ni miradi ya maendeleo.

Matumizi ya kawaida ni pamoja na mishahara, malipo ya mikopo na riba, pensheni, na uendeshaji wa Serikali. Kwa kuzingatia jumla ya mapato ya ndani na misaada ya nje ya shilingi bilioni 4530.0 na jumla ya matumizi ya shilingi bilioni 4,147.4 ya bajeti ya kipindi cha Julai 2007 hadi Machi 2008 ilikuwa na ziada ya shilingi bilioni 282.6

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha huu unaoisha tarehe 30 Juni 2008, Serikali iliendelea na utaratibu wake wa kutumia kulingana na mapato yaliyoko. Utaratibu huu umeonyesha mafanikio makubwa katika kudhibiti matumizi ya Serikali na kuepuka kukopa kutoka soko la fedha la ndani kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi pia imechukua hatua kadhaa za kuboresha zaidi utaratibu huo wa "tumia ulichonacho", katika kutoa fedha kwa watumiaji mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa kuwezesha watumiaji kuwa na maoteo ya mgao wa fedha katika kipindi cha miezi mitatu na kuimarisha Mtandao wa Kompyuta wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha *(IFMS1)* katika ngazi mbalimbali za Serikali. Aidha, Vitengo vya Wizara ya Fedha na Uchumi vya ufuatiliaji wa matumizi vimeimarishwa na vinakagua matumizi ya fedha za Serikali katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa ununuzi wa umma, wakati wa kuwasilisha Bungeni bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/2008, Serikali ilieleza kwamba ilikuwa imetunga Kanuni za Ununuzi wa Umma katika Serikali za Mitaa ili kupunguza matatizo na migogoro ya ununuzi katika Halmashauri mbalimbali.

Kanuni hizi zilichapishwa katika Gazeti la Serikali toleo namba 177 la tarehe 3 Agosti, 2007. Hata hivyo, imedhihirika kwamba, pamoja na kanuni hizo, upungufu wa wanataaluma ya ununuzi ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuviimarisha vitengo hivyo vya ununuzi ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa wataalam wa fani ya ununuzi. Aidha, usimamizi wa taaluma ya ununuzi wa umma inahamishiwa katika Wizara ya Fedha na Uchumi, kutoka Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu umezingatia ukweli kwamba sehemu kubwa ya bajeti ya Serikali inatekelezwa kwa njia ya ununuzi, hivyo kwamba usimamizi wa fedha za Serikali ni pamoja na usimamizi wa Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti matumizi ya Serikali katika ngazi ya Halmashauri, Serikali itapitia upya Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 290, pamoja na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, kwa lengo la kuainisha marekebisho yanayostahili ili kumpa uwezo Mlipaji Mkuu wa Serikali akisaidiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kupeleka madaraka kwa wananchi *(D by D)* katika mwaka 2007/2008, Serikali iliongeza kasi ya kutekeleza sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Serikali zao za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji huo umepitia katika Wizara za Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Kilimo, Chakula na Ushirika; Maji na Umwagiliaji; Afya na Ustawi wa Jamii; Miundombinu; na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na jumla ya shilingi bilioni 216.2 zilihamishwa kwenda kwenye Halmashauri kutoka kwenye Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili liliongeza kiwango cha bajeti za Halmashauri na kufikia jumla ya shilingi trilioni 1.074.6 mwaka 2007/08 kutoka shilingi bilioni 858.4 mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hii ya kupeleka madaraka kwa wananchi, Serikali inaendelea kukabiliana na changamoto ambazo ni pamoja na kujenga uwezo wa Halmashauri ili ziweze kutekeleza kwa ufanisi majukumu yaliyohamishiwa kwao, kuboresha huduma kwa wananchi, kuhakikisha kwamba shughuli zote zinazohamishiwa huko zinapewa rasilimali za kutosha na kuoanisha na kurahisisha taratibu za kupeleka fedha kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara nyingine nane zimefanyiwa tathmini na kuainisha shughuli zitakazohamishiwa kwenye Halmashauri. Wizara hizo ni: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Maliasili na Utalii; Nishati na Madini; Viwanda, Biashara na Masoko na Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa fedha nyingi zinazopelekwa katika Halmashauri zinawafikia walengwa na kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, Serikali itaimarisha ufuatiliaji wa fedha hizo katika ngazi zote, ikiwemo ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali katika mwaka wa fedha 2008/09, itaendelea kuimarisha uwezo wa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Mameya wote nchini ili waweze kusimamia

utekelezaji wa bajeti, kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na usimamizi wa fedha za umma katika mamlaka zao. Serikali pia inatafakari hatua za kuchukua kwa kushirikiana na wadau wengine kupunguza idadi ya akaunti za benki zinazopokea fedha kutoka vyanzo mbalimbali katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha Serikali ya Muungano na ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaendelea na zoezi la kupitia na kuchambua Ripoti ya Tume ya Pamoja ya Fedha kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Kama sehemu ya mchakato huo, Tume ya Pamoja ya Fedha inachambua maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi ya ziada ili kuziwezesha Serikali hizo mbili kufikia maamuzi kuhusu mapendekezo ya Tume.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa bajeti ya 2007/08 hadi 30 Juni, 2008 kwa kuzingatia mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya 2007/08 hadi mwezi Machi 2008, Serikali inaamini kwamba lengo la ukusanyaji wa mapato litafikiwa kama ilivyopangwa ifikapo mwisho wa Juni, 2008. Mapato ya ndani yanategemewa kuvuka kidogo lengo la bajeti la shilingi bilioni 3, 502.583 (trilioni 3.5). Matokeo haya yanatokana na mwenendo wa kuridhisha wa ukusanyaji wa kodi hususani katika vianzio vya VAT na kodi ya mapato. Lengo la mapato ya ndani litafikiwa licha ya ushuru wa forodha na kodi zinazokusanywa kutoka kwenye bidhaa zinazotoka nje na nyingine zisizo za kodi, kutofikia malengo. Misaada na mikopo ya bajeti kutoka nje inatarajiwa pia kuvuka lengo. Hata hivyo, uko wasiwasi kwamba misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo haitapatikana kama ilivyoahidiwa, kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali. Kwa upande wa matumizi, mwelekeo unaonyesha kwamba matumizi ya kawaida yatafikiwa. Matumizi ya maendeleo yanayotegemea fedha za ndani vilevile yatafikia lengo. Matumizi ya maendeleo yanayotegemea misaada ya nje kwa ajili ya miradi hayatafikia lengo.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizo mbele yetu, baadhi ya changamoto za kibajeti ambazo nchi yetu inakabiliana nazo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Mahitaji ya fedha kwa ajili kutekeleza MKUKUTA, hasa ujenzi wa miundombinu ya uchumi na huduma za jamii, ni makubwa sana kuliko uwezo wa Serikali, hata kama mapato yanaongezeka. Zinahitajika juhudi za ziada kuhusisha sekta binafsi ya ndani na ya nje katika kutekeleza MKUKUTA;

(ii) Utegemezi mkubwa wa bajeti kwa misaada ya wahisani, ambayo haitabiriki, unaathiri mipango ya Serikali ya muda wa kati na utekelezaji wa mpango wa kila mwaka. Kwa hiyo, ingawa bado tutahitaji misaada ya nje, ni lazima tuanze mbio ya kujitegemea; *(Makofi)*

(iii) Utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika maeneo ya ununuzi na utoaji wa taarifa za matumizi ya fedha za Serikali, haujaimarika ipasavyo;

(iv) Utekelezaji wa bajeti hasa ya miradi katika sekta za miundombinu unakabiliwa na upungufu wa wakandarasi wenye uwezo, ujuzi, vifaa, na uzoefu wa kutosha. Tatizo hili linahitaji kuwekewa mkakati wa kuliondoa; na

(v) Bei za mafuta ya petroli, vyakula, malighafi, na pembejeo, zikiendelea kupanda zitaathiri bajeti kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, misingi na shabaha ya bajeti ya mwaka 2008/09, Serikali itaendelea kutekeleza malengo ya Kitaifa kama yalivyofafanuliwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2005, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na MKUKUTA. Aidha, mgawanyo wa fedha utaendelea kuzingatia maeneo ya kipaumbele ambayo yataleta msukumo katika uchumi na huduma bora za jamii. Vipaumbele ambavyo vimezingatiwa katika Misingi ya Sera za Uchumi Jumla nilizowasilisha leo asubuhi, ni pamoja na elimu, miundombinu, kilimo, afya, maji na nishati.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Bajeti ya mwaka 2008/09, ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua asilimia 18.5 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 16.7 ya Pato la Taifa mwaka 2007/08;

(ii) Kuzingatia kwa makini vipaumbele vilivyoainishwa kupitia mchakato uliojumuisha sekta zote na wadau wengine na pia katika MKUKUTA, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005, na Malengo ya Milenia;

(iii) Kuanzia mwaka 2008/09, matumizi ya kawaida ya Serikali yatagharamiwa na mapato ya ndani, kwa asilimia mia moja na ushee; *(Makofi)*

(iv) Kuongeza nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali, ikiwa ni pamoja na kusimamia kwa dhati posho ambazo hazina uhusiano na tija na ambazo sio za kisheria; na

(v) Aidha, katika kutekeleza bajeti ya maendeleo umuhimu wa kwanza utakuwa kulipa madeni ya mikataba ya ujenzi, na kukamilisha miradi inayoendelea hasa ya mbiundombinu na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani katika mwaka wa fedha wa 2008/09, yamelengwa kufikia shilingi bilioni 4,728.595 (trilioni 4.728) sawa na asilimia 18.5 ya Pato la Taifa (kwa takwimu za sasa). Hili ni ongezeko la asilimia 31 kutoka mapato yanayotegemewa kukusanywa mwaka 2007/08. Ili kufikia lengo hili kubwa la ukusanyaji wa mapato ya ndani, hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

(i) Mkazo utawekwa katika kupanua zaidi wigo wa kodi, kwa kusajili walipakodi wapya na kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara;

(ii) Wigo wa kodi utapanuka kutokana na kasi ya kukua kwa uchumi hasa katika sekta ambazo zinatoa mchango mkubwa wa mapato ya Serikali. Usimamizi na udhibiti mzuri wa misamaha ya kodi pia utaongeza wigo wa kodi;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa ushuru na kodi katika forodha;

(iv) Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tatu wa Mamlaka ya Mapato *(TRA Third Corporate Plan)* utaongeza uwajibikaji miongoni mwa walipakodi na watoza kodi kadhalika. Mpango huo unataka kuweka mkazo katika ufanisi wa ukusanyaji wa kodi; na

(v) Serikali itaweka taratibu nzuri zaidi za kukusanya mapato yasiyo ya kodi. Matunda ya taratibu hizo yataonekana kuwa ya uhakika kuanzia mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupanuka kwa shughuli za kiuchumi nchini, mapato ya Taasisi, Wakala na Mamlaka za Serikali, yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na kuziwezesha baadhi ya Taasisi hizo kuwa na mapato ya ziada ambayo yangeweza kuchangia mapato ya Serikali. Baadhi ya sheria zilizounda Mamlaka za Udhibiti na Usimamizi wa Umma haziweki bayana nafasi ya Waziri wa Fedha na Uchumi katika usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine za umma, na hivyo uko mgongano kati ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, na zile sheria zilizoanzisha Asasi hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona kuna umuhimu wa Taasisi na Wakala za Serikali na Mamlaka mbalimbali ambazo zinatoza kodi ya huduma kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa kuzingatia hili, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, itafanyiwa marekebisho ili kumpa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuzitaka Asasi hizo kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwaka kulingana na Bajeti za Taasisi hizo. Utaratibu wa kuchangia utaainishwa katika Kanuni za Fedha za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo mipya, Serikali itaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) au J*oint Assistance Strategy for Tanzania (JAST),* kwa lengo la kuboresha mahusiano yetu na nchi wahisani na mashirika ya fedha ya kimataifa. Hatua hii itatuwezesha kuendelea

kupata misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa MKUKUTA.

Hata hivyo, uzoefu katika usimamizi wa misaada umebaini kwamba, wahisani wanachelewa kuthibitisha ahadi zao au wanatoa fedha kidogo kuliko walizoahidi, jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa miradi. Serikali inatafakari njia bora zaidi ya kusimamia misaada ya nje katika muda wa kati ili kuwe na uhakika wa upatikanaji wa fedha zinazoahidiwa na wahisani. Kama nilivyosema awali, kuanzia mwaka wa fedha 2008/09, Serikali imedhamiria kwamba matumizi yote ya kawaida yatatokana na mapato yetu ya ndani. Kwa maana hii, fedha zote za misaada zitaelekezwa kwenye programu na miradi ya maendeleo, kuchochea uchumi kukua kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya ndani kama ilivyokuwa katika mwaka 2007/08, Serikali itaendeleza Sera ya kutokukopa kutoka benki za ndani kupitia soko la dhamana na hatifungani za Serikali kugharamia bajeti yake hasa matumizi ya kawaida. Hata hivyo, dhamana na hatifungani za Serikali zitaendelea kuuzwa katika soko hilo ili kulipia zile zinazoiva *(rollover)* na kusaidia kudhibiti ujazi wa fedha. Aidha, kamati maalum ya usimamizi imeundwa kufuatilia kwa karibu mzunguko wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sera za Matumizi katika mwaka wa fedha 2008/09, Serikali itaendelea kuzingatia sera za matumizi ambazo zimekuwa zikitekelezwa mwaka uliopita, hasa kutoa kipaumbele katika kukuza uchumi, kuboresha huduma za jamii, kupeleka madaraka kwa wananchi, utawala bora, na uwajibikaji, na malengo ya uchumi jumla niliyo yaelezea kwenye Hotuba yangu ya Hali ya Uchumi leo asubuhi.

Aidha, vipaumbele katika bajeti ijayo vimezingatia changamoto zilizoelezwa hapo awali pamoja na maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Vile vile, Serikali itaendelea na utaratibu wa "kutumia tulichonacho" lakini utaratibu huo utaboreshwa. Usimamizi wa matumizi ya Serikali nao utaendelea kuimarishwa kwa kuziba mianya ya matumizi yasiyo na tija kwa kushirikisha ngazi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/09, Serikali imetenga fedha kwenye maeneo mengi muhimu kwa kuzingatia vipaumbele na mipango ya kitaifa niliyoeleza wakati nikiwasilisha Hotuba yangu ya Hali ya Uchumi wa Taifa (mwaka 2007) na mwelekeo wa muda wa kati (2008/09 - 2010/11). Napenda kutaja baadhi ya maeneo yaliyozingatiwa;

Maeneo makuu ya kipaumbele yametengewa fedha kama ifuatavyo:- Sekta ya Elimu imetengewa Shilingi trilioni 1.430 bilioni mwaka 2008/09 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.086 bilioni mwaka 2007/08. Miundombinu ya barabara imetengewa

shilingi bilioni 973.3 bilioni mwaka 2008/09 ikilinganishwa na shilingi bilioni 777.2 mwaka 2007/08. Sekta ya afya imetengewa shilingi bilioni 803.8 mwaka 2008/09 ikilinganishwa na shilingi bilioni 589.9 mwaka 2007/08. Sekta ya Kilimo imetengewa shilingi bilioni 460.0 mwaka 2008/09 ikilinganishwa na shilingi bilioni 379.0 mwaka 2007/08. Sekta ya Maji imetengewa shilingi bilioni 230.6 mwaka 2008/09 ikilinganishwa na shilingi bilioni 309.1 mwaka 2007/08 na Nishati imetengewa shilingi bilioni 383.4 mwaka 2008/09 ikilinganishwa na shilingi bilioni 354.0 mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Spika, sekta hizo sita za miundombinu ya uchumi na huduma za jamii, zimetengewa takribani asilimia 64.8 ya bajeti yote ya 2008/09. Ukiongeza bajeti ya Utawala Bora ambayo ni moja ya maeneo makuu ya MKUKUTA, vipaumbele vya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala na MKUKUTA vitakuwa vimepata fedha zaidi ya asilimia 64 ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa maelezo zaidi kuhusu sekta hizi muhimu, kama ifuatavyo:-

(a) Kilimo kimetengewa shilingi bilioni 460 au asilimia 6.4 ya bajeti ya 2008/09. Aidha, kama nilivyoeleza awali, utekelezaji wa MKUKUTA ni jukumu la Serikali, Sekta binafsi, na wadau wengine wa maendeleo. Ni vizuri pia nieleze kwamba maendeleo ya kilimo yanategemea michango ya sekta nyingine kama vile miundombinu, mikopo na huduma nyingine za fedha, masoko, viwanda na kadhalika.

Katika bajeti ya mwaka 2008/09, sehemu kubwa ya fedha zilizotengwa kwa kilimo zitaelekezwa katika ruzuku ya mbolea, Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(SGR)*, utafiti, hasa wa mbegu bora, na mafunzo. Serikali inategemea kwamba mahitaji mengine ya kilimo kama uzalishaji wa mbolea hapa nchini, na upatikanaji wa matrekta, ni jukumu la sekta binafsi, ikishirikiana na Serikali au Mashirika ya Serikali. Ni muhimu kukumbusha pia kwamba kilimo chetu kitakua cha kisasa chenye tija kama tutakuwa na viwanda vya kusindika mazao na kuacha kuuza nje mazao ghafi. Viwanda vitajengwa na sekta binafsi.

(b) Sekta ya Miundombinu ya barabara imetengewa fedha za kutosha kulipa madeni yote ya mikataba ya barabara na kukamilisha miradi inayoendelea kulingana na mpangilio wa vipaumbele vya Wizara na Halmashauri husika.

(c) Sekta ya Afya imetengewa asilimia 11 ya bajeti ya 2008/09. Ni vizuri nieleze hapa kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya sekta ya afya hazijumuishi zile zinazotolewa na wahisani na mashirika yasiyo ya Serikali nje ya mfumo wa Serikali, kama vile fedha za kupambana na Ukimwi, Malaria na TB na nyingine za namna hiyo ambazo zinasimamiwa na ama wahisani wanaotoa fedha hizo, au wakala wao. Ni vyema pia kukumbusha kwamba asilimia zaidi ya 20 ya huduma za afya zinatolewa na Mashirika ya Dini.

(d) Bajeti ya Maji – inaonekana kushuka ikilinganishwa na mwaka huu wa 2007/08. Sababu kuu ni kwamba ujenzi wa mradi mkubwa wa maji Shinyanga - Kahama, umekamilika. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo za nje zimeendelea kupungua.

(e) Katika bajeti ya Nishati na Madini, ni vyema nieleze kwamba zile fedha zitokanazo na kufutiwa madeni ya IMF (MDRI), ambazo zilitumika kulipia mitambo na jenereta za kuzalisha umeme wa dharura na kulipia chakula kilichoagizwa kutoka nje wakati ule wa uhaba wa chakula sasa zimekwisha. Hivyo miradi katika sekta hiyo sasa itategemea fedha za wahisani pamoja na za kwetu wenyewe.

(f) Kama ilivyokuwa mwaka wa 2007/08, sekta ya elimu imetengewa fedha nyingi kuliko sekta nyingine zote. Hapana ubishi kwamba elimu ndio ufunguo wa maisha. Tumepanua sana fursa za watoto wote wa Tanzania kupata elimu, na tunafahamu kwamba mahitaji ya walimu, vifaa na nyenzo za kufundishia, maabara, chakula, n.k. vinahitajika na ni vya gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo hayo sita ya miundombinu ya Uchumi na Huduma za jamii, liko eneo lingine muhimu la MKUKUTA yaani Utawala Bora, ulinzi na usalama, ambalo lina uzito sawa na yale maeneo sita niliyoyaelezea hapo juu. Yako pia maeneo mengine kama vile malipo ya madeni, pensheni, bima ya Afya, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mwezi Feburari mwaka huu, Rais George W. Bush wa Marekani na Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, walisaini mkataba wa *"Millenium Challenge Compact"* unaotoa msaada kwa Tanzania wa dola za Marekani milioni 698 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya barabara, umeme, maji, na uwanja mmoja wa ndege. Miradi itakayotekelezwa ni ya Tanzania Bara na Visiwani. Mkataba uliosainiwa na Marais hao wawili ni wa miaka mitano. Kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji (2008/09) kiasi kilichotengwa kwenye bajeti ni shilingi bilioni 68.5, kutegemea mpango wa kazi wa utekelezaji wa miradi hiyo ya *"Compact"*.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato. Ili kujenga uwezo endelevu wa kukusanya mapato ya ndani kulipia matumizi yote ya kawaida, Serikali itachukua hatua mbali mbali za kuboresha ukusanyaji wa mapato, ikiweno kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya na kuendelea kuimarisha uchumi tulivu, pamoja na kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji yenye kuiwezesha sekta binafsi kukua. Aidha Mamlaka ya Mapato itaanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tatu wa Maboresho *(Third Corporate Plan)* wa Miaka Mitano, kufuatia kukamilika kwa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maboresho.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kufanyia marekebisho mfumo wa kodi, pamoja na kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, ushuru na tozo zisizo za kodi chini ya Sheria mbali mbali na pia taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Marekebisho hayo yanalenga kuweka mazingira mazuri zaidi ya uzalishaji hapa nchini kupunguza makali ya mfumuko wa bei na kurahisisha ukusanyaji wa kodi. Maboresho hayo yatakuwa chini ya sheria zifuatazo:-

(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani;

(b) Sheria ya Kodi ya Mapato;

(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa;

(d) Sheria zinazosimamia Kodi za Magari;

(e) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(f) Sheria zinazosimamia Mapato yasiyo ya Kodi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya mwaka 148:-

(i) Kurekebisha na kupanua wigo wa huduma zinazotozwa asilimia sifuri ya Kodi ya Ongezeko la Thamani zinapokuwa zimetolewa kwa watumiaji wa nje ya nchi *(export of services)* ili kuhusisha huduma za ushauri wa kitaalam; huduma za mawasiliano ya simu; huduma za kurusha matangazo ya redio na luninga; huduma zinazotolewa na wakala na huduma saidizi za uchukuzi na usafirishaji wa bidhaa. Hatua hii inakusudiwa kutoa motisha zaidi kukuza biashara ya kimataifa katika huduma ili kuongeza mchango wa sekta ya huduma katika fedha za kigeni na katika Pato la Taifa. Inapendekezwa hatua hizi zianze kutumika rasmi tarehe 1 Januari 2009 ili kutoa fursa ya kuandaa kanuni za kuzisimamia;

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta mazito yanayotumika kama nishati ya kupikia (kwa mfano "Moto Poa") ili kuhamasisha wananchi kutumia mafuta hayo badala ya kuni na mkaa kwa matumizi ya nyumbani ili kulinda mazingira;

(iii) Kutoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Special Relief)* kwenye "*ethanol*"; "*dyienstuff*" na "*thickening agent*" zinazoagizwa na kampuni ya Moto Poa kwa ajili ya kutengeneza mafuta mazito ya nishati; *(Makofi)*

(iv) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye gesi asilia iliyosindikwa *(Compressed Natural Gas -CNG)* na mitungi ya kuhifadhia gesi hiyo, kama ilivyo hivi

sasa kwa gesi ya kupikia ya *LPG*, ili kuhamasisha matumizi ya gesi hiyo badala ya mafuta ambayo ni ghali, au mkaa ambao unaharibu mazingira; *(Makofi)*

(v) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye lami (bitumen) ili kupunguza gharama za matengenezo ya barabara; na *(Makofi)*

(vi) Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye magunia yanayotengenezwa hapa nchini kwa ajili ya kuhifadhi nafaka itozwe katika kiwango cha asilimia sifuri. Kwa maana nyingine na yenyewe imesamehewa. *(Makofi)*

Hatua hizi katika Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa pamoja zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,211 milioni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332:-

(i) Kuanzisha kodi mbadala ya mapato kwa kiwango cha asilimia 0.3 ya mauzo ghafi (gross turnover), kwa kampuni zinazoonyesha kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Aidha, kampuni hizi hupata faida ya kibiashara, *(commercial profits)* lakini katika kukokotoa faida inayostahili kulipiwa kodi hujikuta zinaonyesha hasara *(tax loss)* inayosababishwa na vivutio vya uwekezaji ikiwemo viwango vikubwa vya punguzo la gharama za mitaji *(capital expenses)* vinavyoruhusiwa kisheria; *(Makofi)*

(ii) Kuanzisha kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 2 kwa malipo yote ya Serikali kwa wauzaji wa bidhaa na huduma Serikalini wasio na Namba ya Usajili ya Walipa Kodi *(TIN); (Makofi)*

(iii) Kusamehe kodi ya mapato inayotozwa kwenye faida itokanayo na mauzo ya mitaji *(capital gains tax)* kwa vipande kutoka katika mfuko wa uwekezaji wa pamoja ulioidhinishwa *(Approved Collective Investment Schemes);*

(iv) Kufanya marekebisho katika mfumo wa kodi binafsi ya mapato *(Personal Income Tax)* na mapato ya ajira ili kuzingatia ongezeko la kima cha chini cha mshahara Serikalini na kulinda mapato ya ajira dhidi ya athari za mfumuko wa bei. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

**Viwango vya sasa**

**Mapato kwa mwezi** **Kodi kwa mwezi**

| | |
|---|---|
| Shilingi 0 mpaka shilingi 80,000 | Asilimia sifuri. |
| Shilingi 80,001 mpaka shilingi 180,000 | Asilimia 15 ya kiasi kinachozidi shilingi 80,000 |
| Shilingi 180,001 mpaka shilingi 360,000 | Shilingi 15,000 kuongeza asilimia 20 ya kiasi kinachozidi shilingi 180,000 |
| Shilingi 360,001 mpaka shilingi 540,000 | Shilingi 51,000 kuongeza asilimia 25 ya kiasi Kinachozidi shilingi 360,000 |
| Zaidi ya shilingi 540,000 | Shilingi 96,000 kuongeza asilimia 30 ya kiasi kinachozidi shilingi 540,000 |

**Viwango Vinavyopendekezwa**

| **Mapato kwa mwezi** | **Kodi kwa mwezi** |
|---|---|
| Shilingi 0 mpaka shilingi 100,000 | Asilimia sifuri – Hakuna kodi. *(Makofi)* |
| Shilingi 100,001 mpaka shilingi 360,000 | Asilimia 15 ya kiasi kinachozidi shilingi 100,000 |
| Shilingi 360,001 mpaka shilingi 540,000 | Shilingi 39,000 kuongeza asilimia 20 ya kiasi kinachozidi shilingi 360,000 |
| Shilingi 540,001 mpaka shilingi 720,000 | Shilingi 75,000 kuongeza asilimia 25 ya kiasi Kinachozidi shilingi 540,000 |

| | |
|---|---|
| Zaidi ya shilingi 720,000 | Shilingi 120,000 kuongeza asilimia 30 ya kiasi kinachozidi shilingi 720,000 |

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, wananchi wengi watapata mapato zaidi na kulipa kiasi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za Kodi ya Mapato kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 4,353 milioni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta mazito ya *HFO* kutoka Shilingi 117 kwa lita hadi Shilingi 97 ili kupunguza gharama ya uzalishaji viwandani, na kuongeza uwezo wa ushindani wa bidhaa zetu katika soko;

(ii) Kurekebisha mfumo wa kutoza Ushuru wa Bidhaa kwenye magari kutoka mfumo wa sasa wa kutoza ushuru wa asilimia 10 kwa magari yenye ukubwa wa injini unaozidi CC2000 na kuwa na viwango viwili vya asilimia 5 na asilimia 10 kama ifuatavyo:-

(a) Magari yenye ujazo wa ingini usiozidi CC1000 hayatalipa ushuru wa bidhaa; *(Makofi)*

(b) Magari yenye ujazo wa injini unoazidi CC1000 lakini hauzidi CC2000 kiwango cha ushuru kitakuwa asilimia 5 ya thamani ya gari; *(Makofi)*

(c) Magari yenye ujazo wa ingini unaozidi CC2000 kiwango cha ushuru kitakuwa asilimia 10 ya thamani ya gari.

(iii) Kurekebisha kiwango cha ushuru wa bidhaa katika huduma za simu za mkononi kutoka asilimia saba ya gharama ya matumizi ya huduma, hadi asilimia 10 ya gharama hiyo. Sababu kubwa ya rekebisho hili ni kwenda sanjari na mfumuko wa bei *(adjustment for inflation)*;

(iv) Kurekebisha kwa asilimia 12 viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zinazotozwa ushuru huu kwa viwango maalum *(specific rates)*, isipokuwa zile za mafuta ya petroli. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Vinywaji baridi kutoka shilingi 48 kwa lita hadi shilingi 54 kwa lita;
(b) Bia inayotengenezwa na nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, kutoka shilingi 173 kwa lita hadi shilingi 194 kwa lita; *(Makofi)*

(c) Bia nyingine zote, kutoka shilingi 294 kwa lita hadi shilingi 329 kwa lita; *(Makofi)*

(d) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 940 kwa lita hadi shilingi 1,053 kwa lita; *(Makofi)*

(e) Vinywaji vikali, kutoka shilingi 1,394 kwa lita hadi shilingi 1,561 kwa lita.

(v) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 4,775 hadi shilingi 5,348 kwa sigara elfu moja;

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 11,266 hadi shilingi 12,618 kwa sigara elfu moja;

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 20,460 hadi shilingi 22,915 kwa sigara elfu moja;

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara, *"cut filler',* kutoka Shilingi 10,333 hadi shilingi 11,573 kwa kilo; na

(e) Ushuru wa *"Cigar"* unabaki asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazosimamia Kodi za Magari. Inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika kodi za magari:-

(i) Kupunguza viwango vya ada ya mwaka vya leseni za magari kama ifuatavyo:-

(a) Kwa magari yenye ujazo wa ingini usiozidi CC500 kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 30,000 *(Makofi).*
(b) Kwa magari yenye ujazo wa injini unaozidi CC500 lakini hauzidi CC1500 kutoka shilingi 80,000 hadi shilingi 50,000 *(Makofi).*

(c) Kwa magari yenye ujazo wa injini unaozidi CC1500 lakini hauzidi CC2500 kutoka shilingi 150,000 hadi shilingi 120,000 *(Makofi).*

(d) Kwa magari yenye ujazo wa injini unaozidi CC2500 lakini hauzidi CC5000 kutoka shilingi 330,000 hadi shilingi 140,000; na *(Makofi)*

(e) Kwa magari yenye ujazo wa ingini unaozidi CC5000 kutoka shilingi 175,000 hadi shilingi 150,000 *(Makofi)*

(ii) Kusamehe ada ya mwaka ya leseni za magari kwa matrekta ya kilimo. *(Makofi)*

(iii) Kuongeza viwango vya ada ya usajili wa magari kutoka shilingi 27,000 kwa pikipiki na shilingi 90,000 kwa gari, hadi shilingi 35,000 kwa pikipiki na shilingi 120,000 kwa gari. Ada hii inalipwa mara moja tu na mwenye gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi kwa pamoja zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 2,380 milioni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mapendekezo ya marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha yalijadiliwa pamoja na yale ya kutoka Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi katika kikao cha maandalizi ya Bajeti cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichofanyika tarehe 2 mwezi Juni 2008 Jijini Nairobi. Makubaliano ya Mawaziri wa Fedha yatawasilishwa katika Kamati ya Kisekta ya Mawaziri wa Biashara, Fedha na Uwekezaji ili wathibitishe kwa pamoja. Baada ya kuthibitishwa, yatachapishwa katika Tamko la Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, makubaliano hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kusamehe ushuru wa forodha kwenye majembe ya mkono pamoja na pembejeo nyingine zote za kilimo zinazoagizwa kutoka nje ili kupunguza mzigo wa gharama kwa wakulima hasa wale wadogo. Aidha, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inatafiti uwezo wa nchi wanachama kuzalisha pembejeo hizo; *(Makofi)*

(ii) Kusamehe ushuru wa forodha kwenye malighafi na vifaa vinavyoagizwa na kampuni ya *TANELEC* kwa ajili ya kutengeneza mashine za kuongeza na kupunguza nguvu ya umeme, yaani *transformers and switch gears; (Makofi).*

(iii) Kuondoa ushuru wa forodha kwenye shairi itakayoagizwa na kampuni za bia za hapa nchini kwa kiwango kisichozidi tani 20,000 hadi mwisho wa mwezi Desemba 2009;

(iv) Kuondoa ushuru wa forodha kwenye mashine za jamii ya kompyuta, *data processing machines,* zinazotambulika chini ya HSCODE 8443.31.00 na 8443.32.00 kwa kuwa kompyuta hivi sasa hazitozwi ushuru wa forodha;

(v) Kupunguza kiwango cha ushuru wa forodha kwenye madini ya *"Sodium Sulphate"* kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10, ili kupunguza gharama za uzalishaji viwandani;

(vi) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwa magari yaliyotengenezwa maalumu kwa ajili ya ukusanyaji takataka yatakayonunuliwa na Serikali za Mitaa au mawakala walioidhinishwa na Serikali za Mitaa; na *(Makofi)*

(vii) Kuondoa ushuru wa forodha wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula. Mafuta yaliyosafishwa kidogo, *semi-processed*, yataendelea kutozwa ushuru wa asilimia

10. Hatua hii itaviweka viwanda vya mafuta hapa nchini katika nafasi nzuri ya kiushindani na vile vya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi katika Ushuru wa Forodha kwa pamoja zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 762 milioni.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazosimamia Mapato yasiyo ya Kodi. Inapendekezwa kurekekebisha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura ya 348, pamoja na Sheria zinazounda Wakala na Mamlaka za Usimamizi na Udhibiti pamoja na Asasi za Serikali ili kumpa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuzitaka Asasi, Wakala na Mamlaka hizo kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwaka kutokana na mapato ya ziada ya mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Misamaha ya Kodi. Inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuimarisha usimamizi wa msamaha wa kodi unaotolewa kwa mashirika yasiyo ya Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Kurekekebisha kifungu cha 10 cha Jedwali la Tatu ili kuyataka mashirika yanayonufaika na msamaha wa kodi kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato maelezo ya utekelezaji wa, mipango yao ya kazi ya mwaka yakianisha manufaa kwa jamii. Aidha TRA itatoa hati ya stahili ya msamaha, T*ax Clearance Certificate,* itakayowezesha taasisi husika kuendelea kupata msamaha wa kodi.

(ii) Kurekebisha kifungu cha 10 cha Jedwali la Tatu ili kuyataka mashirika yanayonufaika na msamaha wa kodi kuwasilisha uthibitisho kwamba vifaa au huduma zinazoombewa msamaha wa kodi zitatumika katika miradi husika tu na si vinginevyo.

(iii) Kurekebisha kifungu cha 10 cha Jedwali la Tatu ili msamaha unaotolewa chini ya kifungu hiki usihusishe bidhaa za matumizi ya nyumbani, yaani household consumables kama vile glasi, visu na vitu kama hivyo.

(iv) Kufuta kifungu cha 11 cha Jedwali la Tatu la Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kuwa tayari msamaha huu unatolewa katika kifungu cha 10.

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogo madogo katika baadhi ya sheria za kodi. Inapendekezwa kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika Sheria mbalimbali za kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, tarehe ya Kodi mpya kutumika. Hatua hizi mpya za kodi zitaanza kutumika Julai mosi 2008, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Serikali imepanga kupata mapato ya jumla ya shilingi bilioni 7,216.130. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani ni shilingi bilioni 4,728.595 na mapato kutoka kwa wahisani ni shilingi 2,429,535 bilioni. Aidha, Serikali inategemea kupata shilingi bilioni 60 kutokana na uuzaji wa hisa zake asilimia 21 katika benki ya *NMB*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, matumizi ya Serikali yatakuwa shilingi trilioni 7.216 (bilioni 7,216.130). Matumizi ya kawaida yatakuwa shilingi trilioni 4.727 (bilioni 4,726.650, ambayo ni chini ya mapato ya ndani ya shilingi trilioni 4.729 (bilioni 4,728.595). Matumizi ya maendeleo yatakuwa shilingi trilioni 2.489 au 2,489,480 bilioni. Katika matumizi ya maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 1,551.100 kitatokana na fedha za wahisani kupitia miradi pamoja na basketi. Kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 938.380 kitatokana na mchango wa wahisani kupitia misaada ya kibajeti, mapato yatakayotokana na mauzo ya hisa za Serikali pamoja na ziada itakayotokana na mapato ya ndani. Kwa muhtasari, sura ya bajeti inakuwa kama inavyooneshwa katika jedwali nitakalolisoma:-

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani yatakuwa shilingi 4,728,595 kati yake mapato ya kodi yatakuwa 4,497,070 milioni. Mapato yasiyo ya kodi yatakuwa 231,525 milioni. Mikopo na misaada ya nje, ikijumuisha *MDRI* na *Millenium Challenge Cooperation,* itakuwa 2,429,535 milioni. Mauzo ya hisa ya Serikali yatakuwa shilingi 60 milioni.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Kawaida, yote kwa ujumla wake yatakuwa 4,726,650 milioni. Deni la Taifa litakuwa shilingi 648,284 milioni, Wizara 2,478,099 milioni, Mikoa 85,743 milioni, Halmashauri 908,756 milioni, Matumizi maalumu 364,391 milioni, marekebisho ya mishahara ya Serikali shilingi 241,377 milioni.

Matumizi ya maendeleo kwa ujumla wake yatakuwa shilingi 2,489,480 milioni. Fedha za ndani itakuwa 938,380 milioni, fedha za nje kama nilivyosema 1,551,100 milioni.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/09, itatekelezwa katika kipindi ambacho dunia nzima inakabiliwa na changamoto kubwa ya kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli, bei ya nafaka, bei ya pembejeo za kilimo na bei ya malighafi za viwanda. Ongezeko hilo limesababisha kasi ya mfumuko wa bei katika nchi zote duniani.

Aidha, kuvurugika kwa masoko ya fedha ya kimataifa kunaweza kuathiri mtiririko wa vitega uchumi kutoka nchi zilizoendelea kuja nchi zinazoendelea. Kwa hiyo, kunahitajika umakini mkubwa katika kuhimili athari za hali hii ya uchumi wa dunia. Hata hivyo, nchi zinazozalisha mafuta ya petroli zinategemewa kuendelea kunufaika na ongezeko la bei ya mafuta hasa kwa kuwa mahitaji ya nchi kama China, India, na Brazil ni makubwa. Aidha, urari wa malipo ya nje unaonyesha umuhimu mkubwa wa kuweka nguvu zaidi katika kukuza mauzo ya nje ya bidhaa na huduma, ili kuongeza uhimili wa uchumi dhidi ya misukosuko kama hii ya kupanda kwa bei ya bidhaa tunazoagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, kwa upande wa bajeti, changamoto zinazoikabili Serikali ni kutotabirika kwa misaada kutoka kwa wafadhili. Kwa hiyo, tunahitaji kupunguza kasi ya kuongezeka kwa matumizi ya kawaida, hasa yale ambayo hayawezi kurekebishwa iwapo mapato yatapungua. Ili kukabiliana na hali hiyo mambo yafuatayo yatazingatiwa katika mwaka ujao wa fedha:-

(i) Kutekeleza kwa dhati azma yetu ya kupunguza utegemezi wa bajeti yetu kwa wafadhili. Kuanzia mwaka ujao wa fedha, matumizi ya kawaida yatakidhiwa na mapato ya ndani, na kiwango cha utegemezi wa bajeti nzima kwa ujumla kinatarajiwa kupungua hadi asilimia 34 ukilinganisha na asilimia 42 mwaka huu wa fedha 2007/2008. Ukiondoa mikopo ya nje, ambayo italipwa na Serikali, kiwango cha utegemezi kitaendelea kupungua zaidi na kufikia kati ya asilimia 20 na 25 ifikapo mwaka 2010. *(Makofi*)

(ii) Kudhibiti mfumuko wa bei kwa kuimarisha usimamizi wa ujazi wa fedha katika uchumi na kuongeza mashauriano na wadau hasa mabenki ili kuwapa taarifa sahihi za sera za fedha, yaani *Monetary Policy,* utekelezaji wake na muelekeo wake.

(iii) Kuongeza upatikanaji wa nafaka ambazo bei zake zinapanda kwa kasi na kuathiri maisha ya wananchi, ama kusitisha usafirishaji nje wa bidhaa hizo, au kuzitoza kodi ya mauzo nje, au hatua zote mbili kwa pamoja na kuboresha miundombinu hasa ya usafiri vijijini, ili kupunguza gharama za kusafirisha chakula hadi maeneo ya miji; na

(iv) Hatua muhimu kuliko zote ni kutumia ongezeko la bei ya chakula duniani kama fursa ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula hapa nchini, kwa kuhimiza kuwekeza katika mashamba makubwa na kuhimiza wananchi walime chakula kwa wingi ili kujipatia chakula na kipato. Ni vizuri tuitumie changamoto ya upungufu wa chakula duniani kama fursa kubwa ya kuneemeka kwa kuzalisha chakula chetu wenyewe kwa wingi, kwa kuwa ardhi tunayo, watu tunao na hali ya hewa inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*
**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALIIl:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yako hiyo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2008/2009.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitangaze ifuatavyo:-

Kwanza Wageni Mashuhuri. Katika Speaker’s Gallary yupo Mheshimiwa Mama Pinda, mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Yupo pia ndugu Philemon Luhanjo, Katibu

Mkuu Kiongozi, wapo Waheshimiwa Mabalozi na wengine nawaona wanatoka kwa sababu ndege iko karibu kuondoka ambao ni wa kutoka Mozambique, Libya, Malawi, Nigeria, South Africa, France, Angola, Rwanda, Saudi Arabia, India, Uingereza, Zimbabwe, Netherlands, Italia na Indonesia. Wapo Wawakilishi wa Mabalozi kutoka Ubalozi wa Marekani, Kenya na Denmark. *(Makofi)*

Pia wageni wetu Mashuhuri, ni Mkuu wa Majeshi, *CDF*, General Mwamunyange, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspector General, Said Mwema, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, ndugu Othman na Mkuu wa Magereza, Ndugu Nanyaro.

Kwa niaba ya Jaji Mkuu, Jaji Mfawidhi Dodoma, Mheshimiwa Jaji Shangali, Katibu wa Bunge Mstaafu, ndugu Damian Foka. Karibu sana ndugu Damian, tunaendelea kuchota hekima zako katika kuendeleza Bunge hili. Yupo Mzee wetu mmoja wa Mawaziri wa kwanza katika Tanganyika huru, Balozi Sir George Kahama, Mheshimiwa Balozi Mustapha Nyang'anyi, Mwenyekiti wa *Air Tanzania.*

Wapo wawakilishi wa Chama Tawala, CCM, Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi, CUF, Professor Lipumba, Viongozi wa Chama cha *TLP* Mkoa wa Dodoma, Mwakilishi wa Msajili wa Vyama vya Siasa, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa, Kamishna wa Tume ya Maadili, Makamu Mkuu wa Chuo cha Dodoma, ahsante karibu sana.

Yupo pia mama Mkulo, mke wa Waziri wa Fedha, nimeambiwa na watoto wanne, basi nadhani wametoka nje kupata soda. *(Makofi)*

Kamishna Mkuu wa TRA, Mwenyekiti wa Bodi ya TRA, Hongera sana Mwenyekiti wa Bodi na Kamishna Mkuu, kazi mnayoifanya, kwa kweli tunaiona. *(Makofi)*

Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali, tafadhalini msimame waweze kuwaona na kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wengine huku, wengi wako hapa. Ahsanteni sana, karibuni sana Makatibu Wakuu. *(Makofi)*

Manaibu Katibu Wakuu kutoka Wizara ya Fedha, wale pale watatu, wawakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa, the UN System, karibuni sana. Nadhani ndio hawa walioondoka, nadhani inatosha. *(Makofi)*

Tangazo, Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ameniomba nitangaze kwamba wale Waheshimiwa Wabunge, wote wanaokwenda Dar-es-Salaam kesho, mabasi yataondoka hapa nje ya jengo la utawala saa 5:00 asubuhi kuelekea Dar-es-Salaam, kwa ajili ya kuwapa moyo vijana wa Taifa Stars wanaocheza na timu ya Cameroon. Tangazo hili halielezi wanarudi lini, lakini wajue kwamba Jumatatu tuna kazi, tunaanza kujadili hotuba ya Bajeti. Kwa hiyo, natumaini watakuwa wamerejea kabla. Maelezo mengine watapata hukohuko. *(Makofi)*

Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hotuba ya leo, mhakikishe kwamba mwaka huu Wizara ya Fedha imefanya vizuri sana. *Finance Bill* iko tayari na imetawanywa, ambaye hana basi apewe ili unaposoma yaliyomo katika hotuba basi unaona na hatua ambazo zimependekezwa kwa Muswada huu ambao tutaujadili mwishoni mwa mkutano wetu.

Baada ya kusema hivyo, kama ilivyo utaratibu kwa siku kama ya leo, hatuna tena shughuli nyingine na kwa hivyo naahirisha Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 16/6/2008, saa tatu asubuhi mwezi huu.

*(Saa 11.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka*
*Siku ya Jumatatu, Tarehe 16 Juni, 2008*
*Saa Tatu Asubuhi)*